

AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE.....14.11.2017

1. Kufungua Mkutano
2. Kusoma na kuthibitisha Agenda za Mkutano wa Tarehe.....**14.11.2017**
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano wa tarehe.....**22.08.2017**
4. Taarifa ya kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha Julai-Septemba.....**2016/2017**
5. Taarifa ya kamati ya Uchumi,Elimu na Afya Julai-Septemba.....**2016/2017**
6. Taarifa ya kamati ya mipango Miji,Ujenzi na Mazingira Julai-Septemba.....**2016/2017**
7. Taarifa ya kamati ya kudhibiti UKIMWI kwa kipindii cha Julai-Septemba.....**2016/2017**
8. Taarifa za utekelezaji kutoka kwenye kata kwa kipindi cha Julai-Septemba**2016/2017**
9. Kufunga Kikao

**MUHTASARI WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA
UTAMADUNI TAREHE 22.08.2017.**

ORODHA YA WAJUMBE WALIOHUDHURIA KIKAO.

NA	JINA LA MJUMBE	WADHIFA	CHEO
1	Mhe.Twallib S Mangu	Diwani Kata ya Kumsenga	Mwenyekiti
2	Mhe.Deus Kibabi	Diwani Kata ya Ruhita	M/Mwenyekiti
3	Mhe.Anjerina P.Bishikila	Diwani Viti -Maalum	Mjumbe
4	Mhe.Eveline Charles John	Diwani Viti -Maalum	Mjumbe
5	Mhe.Benjamin Chalukura	Diwani Kata ya Nyumbigwa	Mjumbe
6	Mhe.Emmanuel C.Kisunzu	Diwani Kata ya Murubona	Mjumbe
7	Mhe.Amosi F. Mbuyugu	Diwani Kata ya Murufiti	Mjumbe
8	Mhe.Simon F.Njelekela	Diwani Kata ya Muhunga	Mjumbe
9	Mhe.Ayubu N.Kilugu	Diwani Kata ya Kigondo	Mjumbe
10	Mhe.Ezron B.Budulege	Diwani Kata ya Muganza	Mjumbe
11	Mhe.Emmanuel J.Gamuye	Diwani Kata ya Mwilamvya	Mjumbe
12	Mhe.Boniface N. Muhehe	Diwani Kata ya Heru Juu	Mjumbe
13	Mhe.Gilbert Moshi	Diwani Kata ya Kimobwa	Mjumbe
14	Mhe.Jonas Selemani	Diwani Kata ya Kumnyika	Mjumbe
15	Mhe.John H.Mbonye	Diwani Kata ya Nyansha	Mjumbe
16	Mhe.Evance L.Buchonko	Diwani Kata ya Msambara	Mjumbe
17	Mhe.Pili A.Buyogera	Diwani Viti-Maalum	Mjumbe
18	Mhe.Shangwe Yohana	Diwani Viti-Maalum	Mjumbe
19	Mhe.Nelly Nashon Kibamba	Diwani Viti-Maalum	Mjumbe
20	Mhe.Stewart E.Zindutse	Diwani Kata ya Murusi	Mjumbe

WAJUMBE WASIOHUDHURIA

1	Mhe.Daniel Nsanzugwanko	Mbunge Jimbo la Kasulu Mjini	Mjumbe
---	-------------------------	------------------------------	--------

MAHUDHURIO YA WATAALAM.

1	Fatina H.Laay	Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji-Katibu
2	Bw.Charles Bavu	K/Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala
3	Bw.Moshi Munyika	Kaimu Afisa Utamaduni
5	Bw.Zakayo S.Bisakala	Kaimu Mkuu wa Idara Mifugo na Uvuvi
6	Bw.Emmanuel Konkomo	Mkuu wa Idara ya Maji
7	Bw.Revocatus Manyerere	Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
8	Bw.Phaustin Temula	K/Mkuu wa Idara ya Mipango na Ufuatiliaji
9	Bw.Timotheo Mathayo	Katibu wa Kamati
10	Bi.Anitha Pura	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi
11	Bw.James E. Kiptura	Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
12	Bw.Scarion Ruhula	Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Mazingira
13	Bw.Sospiter Alphonse	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA
14	Dr.Eveline Massamu	Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
15	Bw.Sungwa Mkenya	KMkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
16	Eng.Silvanus M.Ngonyani	Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi
17	Bw.Maduhu Kazi.	K/Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji
18	Meshack F.Bilonkwanamagala.	Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika

KAMATI YA ULINZI NA USALAMA

1	Bw.Titus Muguha	Katibu Tawala.....(W)
2	Sospiter Kunguru	Mkuu wa Jeshi la Polisi.....(W)

VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA

1	Bw.Ezekiel B.Kaloba	Mwenyekiti wa CCM (W)
2	Bw.Emma Mteleke	Mwenyekiti NCCR-MAGEUZI
3	Bw.Lucas Gervas Kelegwa	Katibu ACT-WAZALENDO
4	Bw.Bernard Tunguru	Katibu NCCR-MAGEUZI
5	Bw.Nobath Manyonyi	Katibu CCM

WAGENI WAALIKWA

1	Mh.Kanal.Marko Maguti	K/Mkuu wa Wilaya ya Kasulu
2	Titus T.Muguha	Katibu Tawala (W)-Kasulu

VIONGOZI WA DINI

1	Rev.Joseph Thabit	Upendo Harvest
2	Rev.Canon D.Nyugwa	Angilicana
3	Rev.Juma M.Juma	AICT
4	Rev.Gerald Balagomwa	KKKT
6	Sheikh Ramadhani Hussein	BAKWATA

AGENDA NAMBA 01/08/2017-KUFUNGUA KIKAO

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue Mkutano wa Baraza la Madiwani. Mwenyekiti alitumia fursa hii kuwakaribisha wajumbe na kuwasihii kuwa makini katika uchangiaji ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Mwenyekiti alisoma dua la kuliombea baraza la Madiwani na kisha alifungua Mkutano mnamo saa **4:30** za asubuhi. Mwenyekiti aliwathibitishia wajumbe kuwa mawazo, michango na mapendekezo yao yanathaminiwa na yatafanyiwa kazi. Baada ya maelekezo hayo, Mhe.Mwenyekiti alitoa nafasi kwa wageni waalikwa kujitambulisha na wageni waalikwa waliokuwepo siku.

Salamu kutoka serikali kuu

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kasulu alianza kwa kueleza kuwa Hali ya ulinzi na Usalama katika wilaya ya kasulu ni nzuri , changamoto zilizopo ni suala la wahamiaji haramu,jambo ambalo mhe.Mkuu wa wilaya ya kasulu aliwataka wajumbe wote kushirikiana ili kuweza Kupambana na hali hiyo.

Ilijulishwa kuwa kuna mchakato wa kuanza kutoa vitambulisho ili kuweza kuwapatia wananchi fursa ya kuwa na vitambulisho vya uraia.Ushirikiano zaidi unatakiwa ili kuweza kuwabaini wale wote wasiokuwa raia wa Tanzania katika zoezi hili.

Pia aliwataka wajumbe wa Baraza la Madiwani kuongeza ushirikiano zaidi ili kuweza kutekeleza miradi mbalimbali iliyopo katika ngazi ya mtaa hadi kata kama vile ujenzi wa madarasa pamoja na miundombinu mbalimbali kuanzia ngazi ya shule za msingi hadi Sekondari.

AGENDA NAMBA 02/08/2017:-KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE..... 22.08.2017

Agenda 13 za Mkutano wa Baraza la Madiwani zilithibitishwa na kupokelewa kama ifuatavyo hapa chini:-

1. Kufungua Mkutano
2. Kusoma na kuthibitisha Agenda za Mkutano wa Tarehe.....**22.08.2017**
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano wa tarehe.....**02.05.2017**
4. Taarifa ya kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha Aprili-June.....**2016/2017**
5. Taarifa ya kamati ya Uchumi,Elimu na Afya Aprili-June.....**2016/2017**
6. Taarifa ya kamati ya mipango Miji,Ujenzi na Mazingira Aprili-June**2016/2017**
7. Taarifa ya kamati ya kudhibiti UKIMWI kwa kipindii cha Aprili-June.....**2016/2017**
8. Taarifa za utekelezaji kutoka kwenye kata kwa kipindi cha Januari-Machi ...**2016/2017**
9. Taarifa ya Uanizshwaji wa wakala wa Barabara Vijijini na Mijini.....**(TARURA)**
10. Kufunga Kikao

AGENDA NAMBA 03/08/2017:- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA TAREHE.....02.05.2017.

Katibu wa kamati aliwasomea wajumbe Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe **02.05.2017**. Muhtasari huo ulipokelewa na wajumbe na waliridhia kilicho andikwa ndicho kilichojadiliwa kwenye Mkutano huo.Baada ya hapo muhtasari ulisainiwa ili kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao cha tarehe **02.05.2017**.

AGENDA NAMBA 04/08/2017:-TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI KWA KIPINDI CHA APRILI-JUNI... 2017

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kasulu aliwasilisha taarifa ya utekelezaji ya kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha Aprili-Juni 2017. Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa kama inayoonekana hapa chini.

Halmashauri ya Mji-Kasulu kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 ilikisia kupata jumla ya Tshs. **31,620,149,988** ikiwa ni mapato yote ya Halmashauri. -Aidha mapato halisi yasiyo na masharti ni kuanzia Julay hadi June 2017 ni **TZS 936,521,860.51** sawa na asilimia **90.5%** na mapato yenye masharti yaani (Bima ya Afya,Ada ya kila siku na (CHF ni TZS **189,657,973.10** sawa na asilimia **32.3%**. mchanganuo kwa kila chanzo umeoneshwa kwenye jedwali hapa chini:-

S/N	AINA YA MAPATO	KIASI	HALISI HADI JUNI 2017	%
1	Mapato ya ndani kutoka vyanzo mbalimbali	1,035,082,000	936,521,860.51	90.5
2	Mapato ya ndani yenye masharti (Bima ya Afya,Ada ya kila siku na (CHF)	587,200,000	189,657,973.10	32.3
3	Fedha za Fidia ya vyanzo vilivyofutwa	158,866,000	8,770,000.00	5.5
4	Fedha ya Ruzuku ya Maendeleo OC	1,352,782,000	390,447,801.72	28.9
5	Fedha za Miradi ya Maendeleo	7,956,706,200	5,461,431,736.77	68.8
6	Fedha za Mishahara	20,529,513,788	11,926,690,200	58.1
	JUMLA YA MAPATO YOTE	31,620,149,988	18,913,519,572	59.8

Mhe:Mwenyekiti kwa kipindi cha mwezi Juni 2017 Halmashauri ya Mji wa Kasulu ilikusanya mapato ya ndani yenye mashariti-Bima, CHF, USER FEES) kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani (Own sources).

Jumla ya makusanyo yote ya mapato ya ndani yasiyo na mashariti Julai 2016 hadi juni 2017 ni **TZS 936,521,860.51** sawa na asilimia **90.4**.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Kasulu kwa kipindi cha mwezi Juni ilipokea fedha jumla ya **TZS 1,723,777,249.77** .ikiwa ni Ruzuku ya matumizi ya kawaida, mishahara na miradi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao.

- Mapato ya ndani Tshs.....175,703,208.48
- Mishahara Tshs.....1,032,641,100

- TASAF Tshs.....440,000
- Grand high school Tshs.....48,140,941.29
- Fedha zilizokuja na kutakiwa kurudishwa kwenye mfuko mkubwa wa serikali Tshs.....457,895000
- Unicef Tshs.....**8,957,000**

JUMLA KUU Tshs.....1,723,777,249.77

(B) MUHTASARI WA MATUMIZI MWEZI JUNI 2017

S/N	AINA YA MATUMIZI	KIASI	HALISI HADI JUNI 2017	ASILIMIA %
1	Mapato ya ndani kutoka vyanzo mbalimbali	1,035,082,000	860,968,386.95	83.18
2	Mapato ya ndani yenye masharti (Bima ya Afya,Ada ya kila siku na CHF)	587,200,000	170,231,423	28.98
3	Fedha za Fidia ya vyanzo vilivyofutwa	158,866,000	8,770,000	5.5
4	Fedha ya Ruzuku ya Maendeleo OC	1,352,782,000	374,974,650.27	27.72
5	Fedha za Miradi ya Maendeleo	7,956,706,200	4,294,708,613.80	53.98
6	Fedha za Mishahara	20,529,513,788	11,926,690,200	58.10
	JUMLA YA MATUMIZI YOTE	31,620,149,988	17,630,270,574.02	55.76

Mhe.Mwenyekiti hadi kufikia mwezi Juni 2017 Halmashauri ya Mji kasulu ilitumia jumla ya **Tshs 1,602,853,748.70**. kwa machanganuo ufuatao:-

- Mapato ya Ndani Tshs.....317,939,648.06
- Mtumizi mengineyo(OC) Tshs.....12,835,878.
- Mfuko wa Barabara (Road Fund) Tshs.....351,017,235.88
- Fedha za kunusuru kaya Masikini (TASAF) Tshs.....2,417,481
- Idara ya maji Tshs..... 203,229,130
- Mfuko wa Pamoja wa Afya (Busket Fund) Tshs..... 105,819,617
- Fedha za THPS Tshs.....6,374,911
- Unicef Tshs.....11,632,000
- Fedha za CDG mipango Tshs.....14,514,500
- Afya CDG Tshs..... 29,937,000
- Jengo la Halmashauri Tshs..... 383,074,936,52
- GRAND HIGH SCHOOL Tshs.....481,351,055.30
- EQUIP Tshs.....12,207,885
- Mishahara Tshs..... 1,032,641,100

JUMLA Tshs.....1,602,853,748.70

Baada ya wajumbe kupokea na kujadili taarifa ya kamati ya fedha na Uongozi.

AGENDA NAMBA 05/08/2017:-TAARIFA YA KAMATI YA KUDHIBITI VVU/UKIMWI KWA KIPINDI CHA APRILI-JUNI... 2017.

Taarifa ya utekelezaji kazi za kudhibiti **VVU/UKIMWI** kwa kipindi cha Aprili-Juni 2017 ziliwasilishwa na kupokelewa wajumbe kama inayoonyesha hapa chini:-

Shughuli za kuzuia na kudhibiti **UKIMWI** ziliendelea kutolewa kama kawaida katika kipindi cha **Aprili-Juni 2017** kama ifuatavyo:-

- Ushauri na upimaji wa hiari (VCT) –Voluntary Counseling and Testing
- Kutoa huduma za ushauri na upimaji zinazoanzishwa na kuchochewa na watoa huduma wa afya (Provider Initiated Testing and Counselling) (PITC)
- Huduma ya Tiba,Uangalizi na Ufuatiliaji kwa wagonjwa wenye maambuzi ya Virusi vya **UKIMWI** (Care and Treatment).
- Huduma ya kuzuia maambukizi ya **VVU** kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto,(Prevention of HIV from Mother to Child Transmission) (PMTCT).
- Huduma za ugunduzi wa awali wa mtoto waliozaliwa na mama wenye maambukizi **VVU/UKIMWI** chini ya miezi 18 (Early Infant Diagnosis) (Capacity Building)
- Kuendela kuwajengea uwezo watoa huduma wa afya kuhusu stahili kwa walio na maambukizi ya **VVU/UKIMWI** (Capacity Building)
- Kutoa huduma shirikishi za kifua Kikuu na **UKIMWI** (TB/HIV)
- Kutoa huduma kwa wagonjwa wa magonjwa ya ngono na via vya uzazi (STI/RTI)
- Kuendelea kuelimisha jamii kuhusu kujikinga na maambukizi ya **VVU** na Huduma zinazotolewa kwa mtu anayenguduliwa kuwa na maambukizi ya **VVU** na Mahali huduma hizo zinapopatikana.

2. MAFANIKIO.

Halmashauri ya Mji wa Kasulu ilitekeleza afua mbalimbali za **UKIMWI** zikiwa ni pamoja na;

- Kuongezeka kwa uelewa wa jamii katika kujikinga na maambukizi ya **VVU** na **UKIMWI**.
- Kuongezeka kwa uelewa wa jamii juu ya matumizi sahihi ya kondomu na dawa za kupunguza makali ya **VVU**.
- Kupungua kwa unyanyapaa miongoni mwa jamii kwa watu wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya **UKIMWI** na Ukimwi.
- Kuongezeka kwa hamasa kwa jamii kutaka kujua afya zao juu ya maambukizi ya Virusi vya **UKIMWI** na Ukimwi.

- Pamoja na mapungufu mbalimbali kujitokeza, kwa ujumla zoezi lilienda vizuri na kufanikiwa zaidi katika maeneo mengi, hivyo tunategemea mafanikio zaidi juu ya udhibiti wa UKIMWI katika wilaya ya Kasulu.

1.3: CHANGAMOTO.

- Mwitikio hasi wa jamii (hasa akina Baba) kushindwa kuhudhulia katika dhana nzima ya kuzuia maambukizi ya Virusi vya UKIMWI Kutoka kwa mama kwenda kwa Mtoto(Huduma ya PMCTC).

1.4: UTATUZI WA CHANGAMOTO

Kuendelea kuhamasisha wakina mama kuja na waume zao pindi wanapokuja kuanza clinic katika kipindi cha ujauzito ili kuweza kudhibiti maambukizi ya Virusi vya **UKIMWI** kutoka kwa mama kwenda Mtoto. Baada ya agizo hilo kutolewa , wajumbe walipongeza kwa taarifa hiyo iliyowasilishwa na Mhe.Mwenyekiti wa kamati husika, ambaye ni mheshimiwa **Deus Kibabi**.

AGENDA NAMBA 06/08/2017:-TAARIFA YA KAMATI YA MIPANGO MIJI, UJENZI NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA APRILI-JUNI....2017.

Mwenyekiti wa kamati ya Mipango Miji, Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa kipindi kwa kipindi cha Aprili-Juni 2017 kama inayoonekana hapa chini

Idara ya Usafi na Mazingira

Idara ya Usafi na Mazingira ina vitengo viwili; Kitengo cha usafi na kitengo cha Mazingira. Kitengo cha Usafi kina majukumu ya kusimamia usafishaji wa mji, ukaguzi wa majengo ya vyakula, ukaguzi maeneo ya wazi, mifereji ya maji ya mvua , utunzaji, uchambuzi na usafirishaji wa taka ngumu . Kitengo cha Mazingira kina majukumu ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira (ardhi, maji, hewa na sauti), utunzaji wa mazingira na upandaji miti, majani na maua na kufanya tathmini ya athari za mazingira katika miradi ya maendeleo.

Jumla ya kata zote za Halmashauri ya Mji wa Kasulu 15 zilishindanishwa juu ya kampeni ya usafi wa mazingira Kitaifa. Kata tatu (3) za Murubona, Nyansha na Murusi zilionekana kutimiza baadhi ya vigezo vilivyoko kwenye mwongozo wa kampeni ya mashindano ya usafi wa mazingira kwa mwaka 2016/2017.

Katika kipindi cha robo ya nne yaani Aprili-Juni, 2017, Halmashauri kupitia Idara ya Ujenzi imetekeleza miradi mbalimbali ya barabara kulingana na bajeti ya mwaka 2016/2017. Miradi hiyo itaigharimu Halmashauri jumla ya Tshs.763,289,200.00 .Hadi tarehe 30 Juni 2017 miradi hiyo ilikuwa katika hatua mbalimbali ya utekelezaji. Katika kipindi hicho cha Aprili-Juni 2017,

Halmashauri imepokea fedha kutoka Mfuko wa Barabara jumla ya Tshs.91,000,637.82 tu kutoka OR-TAMISEMI fedha hizo ni za bajeti ya mwaka 2016/2017.

Aidha Halmashauri kupitia Idara ya Ujenzi kwa kushirikiana na idara ya Elimu Sekondari imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya majengo ya shule ya sekondari Bogwe ambapo kuna ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64 kila moja kwa jumla ya Tshs.75,000,000.00 kila moja na Ujenzi wa miundo mbinu mbalimbali katika shule tarajiwa ya kigoma Grand High School kwa jumla ya Tshs.1,000,000,000.00.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa , wajumbe walipongeza kwa taarifa hiyo iliyowasilishwa na Mhe. Mwenyekiti wa kamati husika, ambaye ni mheshimiwa **Emmanuel C.Kisunzu**.

AGENDA NAMBA 07/08/2017:-TAARIFA YA KAMATI YA UCHUMI, ELIMU, AFYA NA MAJI KWA KIPINDI CHA APRILI-JUNI.....2016/2017.

Mhe:**Gilbert Moshi** Mwenyekiti wa kamati ya Uchumi, Elimu, Afya na Maji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi kwa kipindi cha Aprili-Juni **2017**. Taarifa iliwasilishwa na kujadiliwa wajumbe wa mkutano wa Baraza la Madiwani.

Idara ya Maendeleo ya Jamii

Idadi ya vikundi vilivyosajiliwa katika robo ya nne ni kama ifuatavyo:- Mwanamke wekeza - Nyansha, Tuhudumiane wajane Nyansha, TukoImara–Kimobwa, Umamwi Mwilamvya, Niyonkuru -Kumnyika, Umoja na maendeleo, nishikemkono–Murusu, Bwiza–Murusu, Amani Kibagwe, Umoja wa wafuganyuki-Herujuu, Amani - Ruhita. Jumla ya vikundi vilivyosajiliwa ni 11.

CHANGAMOTO

1. Bidhaa nyingi za Kasulu hazina nembo ya TBS kwa kuwa sido ndiyo mwenye jukumu la kuelekeza wajasiliamali jinsi ya kuongeza thamani na kuwaunganisha na taasisi ya TBS kwa ajili ya bidhaa zao.

UTATUZI WA CHANGAMOTO

2. Idara ilifanya mawasiliano na SIDO kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo kwa wajasiliamali ili wajue taratibu za kufuata bidhaa zao ziweze kuuzwa ndani na nje ya Kasulu. Mpaka sasa sido ilitoa majibu kuwa watakuja kutoa mafunzo tangu mwaka jana mwezi wanne hadi sasa hakuna utekelezaji. Hili ni hitaji kwa vikundi mbalimbali vya wazalishaji mali na wajasiliamali.

Idara ya Elimu Msingi

Halmashauri ya Mji wa Kasulu ina jumla ya shule za Msingi 59 za serikali zenye jumla ya wanafunzi 55,322 kati yao wavulana 27448 na wasichana 27,874. Katika kipindi cha mwezi April – Juni **2017** Idara ya Elimu Msingi imefanya kazi zifuatazo:- Kuendelea kutoa huduma za kitaalamu na kitaalamu kwa wateja mbalimbali wanaofika ofisini.

Kuendelea kusimamia utekelezaji wa sera ya ‘**ELIMU BILA MALIPO**’ kwa wanafunzi wote wa Elimu ya msingi. Fedha zilizoletwa kwa ajili ya Elimu Bila Malipo kwa mwezi April – Juni 2017 ni kama ifuatavyo:-

MGAWANYO WA FEDHA ELIMU BILA MALIPO APRIL-JUNE 2017

NO	MWEZI	KIASI
1	APRIL	34,795,000
2	MAY	34,422,312.24
3	JUNE	34,795,000
	JUMLA	104,012,312.24

Aidha taarifa ya kila idara ziliziwasilisha taarifa zake katika kamati hii zilipokelewa na hazikuwa na mjadala.

Baada ya maelekezo hayo kutolewa , wajumbe walipongeza kwa taarifa hiyo iliyowasilishwa na Mhe. Mwenyekiti wa kamati husika, ambaye ni mheshimiwa **Gilbert M.Moshi**.

AGENDA NAMBA 08/08/2017:-KUWASILISHA TAARIFA ZA KATA KUTOKA KWENYE KATA ZOTE ZA KASULU MJINI KWA KIPINDI CHA APRILI-JUNI 2017.

Taarifa za utekelezaji kazi kutoka kwenye kata kwa kipindi cha **Aprili-Juni 2017** ziliwasilishwa na kupokelewa. Katika kujadili wajumbe walipongeza kwa utekelezaji taarifa hizo ambazo ziliwasilishwa kutoka katika kata za zote zilizopo Halmashauri ya Mji-kasulu. Kata ya Murubona, Kumnyika, Nyansha, Muganza, HeruJuu, Nyumbigwa, Kigondo, Ruhita, Msambara, Mwil aamvya , Murusi, Muhunga, Murufiti, kumnyika, kimobwa pamoja na kumsenga.

Ushauri.

Iliashauriwa kuwa Idara ya Mipango na Ufuatiliaji ikazifanyie uchambuzi taarifa hizi za kata ili kuweza kutazama changamoto zilizopo katika taarifa hizo..Uchambuzi ufanyike na changamoto zimeendelea kufanyiwa kazi kadri ya fedha zinavyopatikana.

AGENDA NAMBA 09/08/2017:- TAARIFA YA UANIZSHWAJI WA WAKALA WA BARABARA VIJIJINI NA MIJINI.....(TARURA).

Katibu wa kikao cha baraza la Madiwani aliwasilisha taarifa ya uanzishwaji wa wakala wa Barabara Vijijini na Miji (**TARURA**) na wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuipongeza serikali kwa hatua za uanzishwaji wa mamlaka hiyo ya Barabara Vijijini na Mijini. Ila wajumbe walitaka kufahamu jinsi miradi ya barabara iliyokuwa imetengewa fedha kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 jinsi itakavyoendelea kutekelezwa.

Katibu aliwajulisha wajumbe kuwa miradi hiyo itaendelea kutekelezwa kupitia wakala wa Barabara (**TARURA**) kama ilivyopangwa kwenye bajeti ya Halmashauri ya Mji kwa mwaka wa fedha **2017/2018**.

Aidha katibu alitoa ufafanuzi kuwa uhitaji wa barabara zetu utatoka katika kata zetu na wakala wa barabara atazipitia na kuzipeleka kwenye kikao cha **Bodi** ya Barabara kwaajili ya kuzijadili baada ya wao kujiridhisha kuwa barabara hizo zinahitaji kufanyiwa Matengenezo.

AGENDA NAMBA 10/08/2017:-KUFUNGA MKUTANO

Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa michango yao mizuri kisha alikifunga kikao mnamo saa 9:30 za alasiri.

MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA.....

.....
KATIBU
.....

SAINI

.....
MWENYEKITI
.....

SAINI

TAREHE.....

HALMASHAURI YA MJI KASULU
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Simu/Fax 255-028-2810355

S.L.P. 475.
14.11.2017

Mhe: Mwenyekiti

Mkutano wa Baraza la Madiwani



MJI- KASALU.

**YAH: TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI KATIKA KIPINDI CHA (JULAI-
SEPTEMBER 2017) KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018).**

Mhe Mwenyekiti ifuatayo ni taarifa ya kamati ya kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha Julai-
Septemba 2017. Aidha kamati hii inaundwa na idara zifuatazo:-

- Idara ya Fedha na Biashara
- Idara ya Utumishi na Utawala
- Idara ya Mipango na Ufuatiliaji
- Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
- Kitengo cha Manunuzi na Ugavi
- Kitengo cha Sheria
- Kitengo cha TEHAMA

Mhe. Mwenyekiti Mhutasari wa taarifa ya kazi kwa kila idara umeambatanishwa katika taarifa hii.

Naomba kuwasilisha.

Mh.Deusi Kibabi

Makamu Mwenyekiti

Halmashauri ya Mji- KASULU

Idara ya fedha na Biashara

- Halmashauri ya Mji-Kasulu kwa Mwaka wa fedha 2017/18 ilikisia kupata jumla ya **TZs.35,589,811,380.00** ikiwa ni mapato yote ya halmashauri. Pamoja na bajeti hiyo iliyopitishwa, halmashauri ya mji wa Kasulu ilikuwa na bakaa ya fedha **TZs.1,215,934,820.00** zilizovuka mwaka wa fedha 2016/17 na kufanya jumla ya bajeti ya Halmashauri kuwa **TZs 36,805,746,200.00**. Mchanganuo wa bajeti na fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai-Septemba ni kama ifuatavyo:-

S/N	AINA YA MAPATO	BAKAA 2016/17	MAKISIO 2017/18	JUMLA YA MAKISIO 2017/18	HALISI HADI SEPTEMBER 2017	%
1	Mapato ya ndani yasiyo na masharti	6,670,619.00	1,244,869,000.00	1,251,539,619.00	254,425,041.00	20.4
2	Mapato ya ndani yenye masharti	0	600,070,000.00	600,070,000.00	78,050,060.00	13.0
3	Fedha za Fidia ya vyanzo vilivyofutwa	0	64,301,000.00	64,301,000.00	00	00
4	Fedha ya Ruzuku Matumizi ya kawaida	362,960.79	677,817,000.00	678,179,960.79	134,711,600.00	19.9
5	Fedha za Miradi ya Maendeleo	1,197,733,526.02	12,832,867,380.40	14,030,600,906.42	742,802,140.00	5.8
6	Fedha za Mishahara	11,167,714.10	20,169,887,000.00	20,181,054,714.10	2,817,519,100.00	14
	JUMLA YA MAPATO YOTE	1,215,934,820	35,589,811,380	36,805,746,200	4,027,507,941.00	11.3

Jumla ya makusanyo yote ya mapato ya ndani yasiyo na masharti kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai-Septemba 2017 ni **TZS 254,425,041.00** sawa na asilimia **20.4**

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Kasulu kwa kipindi cha Julai - Septemba imepokea fedha jumla ya **TZS 4,027,507,941.00** ikiwa ni mapato ya ndani, Ruzuku ya matumizi ya kawaida, mishahara na miradi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:

- Mapato ya ndani (Masharti na isiyo ya masharti) Tshs.....332,475,101.00
- Mfuko wa lipa kulingana na matokeo(RBF) Tshs..... 90,000,000.00

- Matumizi ya kawaida OC Tshs.....134,711,600.00
- Ruzuku ya mishahara Tshs.....2,817,519,100.00
- Mfuko wa Jimbo Tshs.....22,148,500.00
- Mfuko wa TASAF Tshs.....318,917,440.00
- Kigoma Grand High School Tshs..... 300,000,000.00
- Shirika la kuboresha na kuwezesha
Huduma za afya(THPS) Tshs..... 11,736,200.00

JUMLA KUU TSHS..... 4,027,507,941.00

(B) MUHTASARI WA MATUMIZI ROBO YA KWANZA HADI SEPTEMBER.....2017

S/N	AINA YA MATUMIZI	BAKAA 2016/17	MAKISIO 2017/18	JUMLA YA MAKISIO 2017/18	HALISI HADI SEPTEMBER 2017	%
1	Mapato ya ndani yasiyo na mashari	6,670,619.00	1,244,869,000.00	1,251,539,619.00	154,037,778.53	12.3
2	Mapato ya ndani yenye masharti na mashari	0	600,070,000.00	600,070,000.00	45,340,106.43	7.6
3	Fedha za Fidia ya vyanzo vilivyofutwa	0	64,301,000.00	64,301,000.00	00	00
4	Fedha ya Ruzuku Matumizi ya kawaida	362,960.79	677,817,000.00	678,179,960.79	107,440,000.00	14.5
5	Fedha za Miradi ya Maendeleo	1,197,733,526.02	12,832,867,380.40	14,030,600,906.42	695,851,985.24	5.4
6	Fedha za Mishahara	11,167,714.10	20,169,887,000.00	20,181,054,714.10	2,817,519,100.00	13.4
	JUMLA YA MATUMIZI YOTE	1,215,934,820.00	35,589,811,380.00	36,805,746,200.00	3,820,188,970.20	10.7

- Halmashauri inaendelea na Ujenzi wa Soko la Sofya ambapo kwa sasa umefikia hatua ya upauaji kwa baadhi ya shedi . Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Ruzuku ya Maendeleo (LGCDG). Katika chanzo cha fedha cha Ruzuku ya Maendeleo kiasi cha Tshs.**100,000,000/=**kilipokelewa

kwa mwaka **2016/2017**. Makadrio yaliyohuishwa kwa kazi hiyo yanaonesha kuwa jumla ya Tshs.**98,092,600/=**zinahitajika zaidi ili kuweza kukamilisha mashed 5 katika soko hilo.Hivyo wajumbe wa kamati ya fedha na uongozi walipendekeza kuwa mradi wa soko la sofya ukamilishwe na mapato ya ndani kwa kiasi kinachohitajika cha Tshs.**98,092,600/=**.

- Taarifa ya kuomba kununua genereta ya dharula ya Hospitali ya Mji wa Kasulu.Hospitali ya Mji imekumbwa na ukosefu wa genereta kwa muda wa miezi mitatu kwani genereta iliyokuwepo iliharibika na mafundi walibainisha kuwa genereta hiyo haiwezi kutengenezeka. Hivyo wajumbe wa kamati ya fedha na Uongozi waliridhia ombi la kununua genereta nyingine itakayogharimu kiasi cha Tshs.**58,000,000/=** Hivyo ilipokea ombi la fedha kiasi cha Tshs. **30,000,000/=** kwaajili ya ununuzi wa genereta kutoka kwenye mapato ya hospitali na fedha nyingine kiasi cha Tshs. 28,000,000 kitagaharamiwa na Halmashauri. Genereta inayohitajika ni **CATEPRILLAR KVA 80AV/100**.

Idara ya Mipango na Ufuatiliaji

- Idara ya Mipango na Ufuatiliaji ilifanya kazi za Ufuatiliaji wa miridi inayoyekelezwa katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Afisa Mipango aliwalisisha taarifa kuwa kwa mwaka 2017/2018 halmashauri inatarajia kupokea fedha Kiasi cha TZS 13,286,968,780.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Fedha hizo zinategemewa kutolewa na Serikali Kuu, Wafadhili na Mapato ya Ndani.
- Katika Kipindi cha Julai – Septemba, 2017 ilipokea jumla ya Tshs. 724,803,295.09 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Mchanganua wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali hapa chchini:-
-

S/NA	AINA YA MRADI	KIASI KILICHOPOKELEWA	HATUA YA UTEKELEZAJI
1	Kigoma Grand High School	300,000,000	Kazi inaendelea na ujenzi upo hatua mbalimbali
2	Lipa kutokana na matokea (RBF) Afya kwa kituo cha Afya cha Kiganamo, na Zahanati za Kanazi, Kidyama, Kigondo, Muhunga, Heru Juu, Mwibuye, Mwanga na Murufiti	90,000,000	Fedha zimehamishwa kwenda kwenye kituo cha Afya 1 zahanati 8 na kila zahanati TZS 10,000,000/= na kazi za ukarabati zinaendelea.
3	TASAF	155,170,720.00	Fedha zimeshapekwa kwa walengwa wa kaya maskini
4	Mfuko wa Jimbo	22,148,500	Kikao cha mfuko kimeshaka na fedha zipo kwenye mchakato wa kuhamisha kwenye

			miradi ilipendekezwa kupata fedha hizo.
5	Elimu bila malipo kwa shule za msingi na Sekondari	145,143,380.00	Fedha zimepelekwa shuleni moja kwa moja
6	Mapato ya ndani	63,656,000.00.	Fedha Kiasi cha Tshs. 63,656,000.00 kimetolewa kutoka katika chanzo cha Mapato ya Ndani kwa ajili ya Miradi ambapo, miradi ya ukarabati wa machinjio, ukarabati wa vyumba vya maabara – Kinkati Sekondari, malipo ya deni la matengenezo ya barabara Kabanga, kutoa mafunzo ya mfumo ulioboreshwa wa Planrep, na kuchangia ujenzi wa Kigoma Grand High School imetekelezwa.
		776,118,600	

• **FEDHA ZA MIRADI ZILIZOPOKELEWA MOJA KWA MOJA SHULENI**

S/NA	CHANZO CHA FEDHA	KIASI KILICHOPOKELEWA	HATUA YA UTEKELEZAJI
1	Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na vyoo matundu 6 shule ya msingi Mwilamvya -Miradi ya P4R	66,600,000.00	Mradi huu umefikia hatua ya umaliziaji na kazi inaendelea.
2	Mradi wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na vyoo matundu 6 katika shule ya msingi Mwibuye.	66,600,000.00	Ujenzi unaendelea na ujenzi upo hatua madarasa ipo katika hatua za usafi na vyoo ipo kwenye hatua ya kufunika shimo.
3	Ujenzi wa chumba cha maabara na ukamilishaji wa vyumba 5 vya madarasa katika shule ya sekondari Mubondo	57,380,000.00	Fedha kiasi cha Tshs 57,380,000.00 zimepokelewa katika shule ya sekondari ya Mubondo kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha maabara (Tshs. 50,000,000), umaliziaji wa vyumba vitano vya madarasa (Tshs. 7,380,000.00). Chumba cha maabara kimekamiliwa. Vyumba

			vya madarasa vimeezekwa na vimefikia upigaji wa lipu umefanyika.
4	Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa shule ya sekondari Muka, matundu ya vyoo sita na mabweni mawili.	216,600,000.00	Fedha kiasi cha Tshs 216,600,000.00 zimepokelewa katika shule ya sekondari ya Muka kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa ambavyo vimefikia hatua ya ukamilishaji. matundu ya vyoo sita (6) hatua ya ukamilishaji na mabweni mawili (2) ambayo yapo katika hatua ya lenta.
	Jumla	407,180,000	

Idara ya Utumishi na Utawala

- Kikao cha kamati ya fedha kilipokea taarifa ya kikao cha Bodi ya Ajira kilichofanyika tarehe 19 septemba 2017 baada ya kupokea taarifa ya wito toka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji. Kama mnavyofahamu Halmashauri ilipokea kibali cha Ajira Mbadala kwa watendaji wa mitaa na vijiji kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora kwa barua yenye Kumb Na. CFC.26/205/01 “FF” ya tarehe 22 Agosti, 2017. Halmashauri iliandaa Tangazo la nafasi hizo tarehe 25 Agosti, 2017 na mwisho wa Maombi ilikuwa tarehe 08 Septemba,2017. Tarehe12-13 Septemba, 2017 Halmashauri ilifanya uchambuzi wa maombi yote 47 yaliyowasilishwa ofisini kwa Mkurugenzi, Waombaji waliokidhi vigezo walijulishwa tarehe 14 Septemba 2017 ili wafike kwa ajili ya usaili uliofanyika tarehe 19 Septemba, 2017. Aidha walioitwa kwenye usaili ni ; Mussa Patrick, Aneth Nicholas Lutera, Marry Nicholas Ruhamvya na Bi. Beatha Evarist.
- Matokeo ya Usaili yalikuwa Kama ifuatavyo, Mussa Patrick alipata 67.25%, Mary Nicholas Ruhamvya 63.25%, Aneth Nicholas Lutera 63% na Bi Beatha Evarist 53.75%. Hivyo Bw. Mussa Patrick alishinda usaili kama matokeo yanavyoonesha.
- Katika kipindi cha robo ya tatu, Idara ya Utawala na Utumishi imeendelea kusimamia shughuli mbalimbali zikiwemo za kiutawala na kiutumishi kwa ujumla katika ngazi ya ofisi na hadi ngazi ya kata na mitaa.Hata hivyo imeendelea kusimamia maadili na nidhamu ya watumishi mahali pa

kazi,masilahi mbalimbali kama likizo,Uhamisho na stahili zingine za watumishi zilizopo kwa mujibu wa sheria,kanuni na tararibu za utumishi wa Umma.

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

- Katika kipindi cha robo ya nne yaani Aprili hadi Juni 2017, Kamati ilipitia taarifa ya ukaguzi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani za Halmashauri. Katika kipindi hicho Kitengo cha Halmashauri kupitia Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, imeendelea kutekeleza ukaguzi katika Idara na Vitengo vyote vya Halmashauri katika Akaunti zote za Halmashauri,kama Akaunti ya Matumizi Mengineyo (Other Charges (OC),Akaunti ya barabara (Road Fund A/C), Akaunti ya Amana (Mesceleniuos A/c), Akaunti ya Maendeleo (Development A/C), Akaunti ya mapato ya Ndani (Own source A/C), Miradi inayotekelezwa na Halmashauri kwa mwaka wa Fedha ya mwaka 2016/2017. Hata hivyo Kitengo cha Ukaguzi kimeendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuhakikisha kuna kuwepo na thamani ya fedha kwa miradi inayotekelezwa .Aidha kitengo kinafanya kazi ya ufuatiliaji mifumo yote ya malipo na kuhakikisha kuna kuwepo uthibiti ubora na matumizi katika serikali .

Kitengo cha Sheria

- Katika kipindi cha mwenzi Julai hadi Septemba 2017, Kitengo Cha Sheria katika Halmashauri ya Mji Kasulu kimetekeleza shughuli zifuatazo:-Kuendesha mashauri mbalimbali katika Mahakama mbalimbali ikiwa ni pamoja na Baraza la ardhi na Nyumba la Wilaya Kigoma na Tume ya Usuluhishi Kigoma (C.M.A) na Mahakama Kuu Tabora. Kupeleka Sheria ndogo TAMISEMI kwa ajili ya upekuzi ili ziweze kutangazwa kwenye Gazeti la serikali.

Kitengo cha sheria kilifanikiwa kupeleka sheria ndogo TAMISEMI kwa ajili ya upekuzi ili zitangazwe kwenye Gazeti la serikali na kuanza kutumika katika halmashauri ya mji wetu.Sheria hizo ni kama ifuatavyo:-. Sheria ndogo ya Kodi ya majengo za halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka /2017,Sheria ndogo za Usafi wa mazingira za Halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka /2017,Sheria ndogo za (Ushuru wa Stendi) za Halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka /2017. Sheria ndogo za (Ushuru na kodi za madini ya ujenzi)) za Halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka 2017. Sheria ndogo ya (Uanzishwaji wa mfuko wa afya ya jamii) za Halmashauri ya Mji wa Kasulu za mwaka 2017.

Kitengo cha Manunuzi

- Kitengo cha manunuzi kimefanya manunuzi ya mikataba midogo (LPO) yenye jumla ya TZS.218,472,868/=na kati ya hizo kiasi cha TZS.201,719,218/= kilikuwa kimelipwa.
- Kamati ya fedha na Uongozi ilifanya mabadiliko ya Katibu wa Bodi ya zabuni kwakuwa mkuu wa kitengo cha Ugavi na Manunuzi ameripoti . Kwani hapo awali Katibu alikuwa Bi. Anitha Pura ambaye alikuwa kaimu Mkuu Wa Kitengo lakini kwa Sasa Ameripoti Mkuu wa Kitengo ambaye ni Bw. Felix Mkriya. Hivyo Bw. Felix Mkriya achukue nafasi ya Bi Anitha Pura na kuwa katibu wa Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Mji-Kasulu.

- Kamati ya Fedha na Utawala ilihitaji kufanyika kwa uchunguzi ili kubaini kama kulikuwa na maslahi binafsi kwa Watumishi ambao ni wajumbe wa Timu ya Tathmini (Evaluation Team). Uchunguzi ulifanywa na Taasisi ya kuzuia na Kupambana na Rushwa. Matokeo ya Uchunguzi ni kama ifuatavyo;
 1. Uchunguzi haukuthibitisha kama kulikuwa na Masilahi Binafsi miongoni mwa Watumishi katika hatua mbalimbali.
 2. Uchunguzi umebaini kuwa wapo Watumishi wasio Waadilifu ambao ni wajumbe wa **PMU**
 3. Uchunguzi umebaini kuwa hakukuwa na kukiukwa kwa baadhi ya Taratibu.

Kufuatia uchunguzi uliofanyika, Mambo yafuatayo yaliweza kupendekezwa:-

1. Maamuzi ya kikao cha Bodi ya Zabuni ya tarehe 26/07/2017 yaliyotoa ushindi kwa Bw. **M/S DAKAMU INVESTMENT** yazingatiwe.
2. Ofisi ya Mkurugenzi itafute namna ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uongozi ili wafahamu mipaka yao ya kiutendaji katika kushughulikia masuala ya manunuzi ya Umma. Baada ya kupata taarifa ya uchunguzi, kikao kiliridhia kuwa **DAKAMU INVESTMENT** aendelee kuwa Mzabuni wa usafi wa Mji.

Idara ya Mipango na Ufuatiliaji

Kitengo cha TEHEMA

- Katika robo hii ya nne, kitengo kimeweza kushirikiana na Mafundi wa TTCL kwa ajili ya kufunga Mkongo wa *Optical Fiber Cable (OFC)* kwa ajili ya kupitisha mifumo kutoka Ofisi za TTCL mpaka Ofisi za Halmashauri ya Mji Kasulu. Kufunga Rack cabinet katika ofisi ya TEHAMA kwa ajili ya kusimika fiber, Kuondoa kwenye DOMAIN ya Kasulu DC vifaa vyote vya mifumo ya EPICOR na LGRCIS ,Kuamisha vifaa vya mifumo ya EPICOR na LGRCIS KUTOKA Kasulu DC na kuja Kasulu TC, Kuwekea program anzishi na program huishi kompyuta moja ya Idara ya Fedha baada ya kugoma kuiunganisha kwenye Kusimamia na kufanya settings katika mfumo wa TASAF ili viweze kuwasiliana na server ya TASAF Makao makuu. Kutoa mafunzo ya mfumo wa barua pepe za serikali, *government mailing system(gms)* kwa wakuu idara na vitengo kwa kuwafuata mahali pao pa kazi katika ofisi zao, pamoja na kuwakabidhi barua pepe za serikali kwa ajili ya mawasiliano ya ki-serikali.

HALMASHAURI YA MJI KASULU
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Simu/Fax 255-028-2810355



S.L.P. 475.

Mhe: Mwenyekiti

Mkutano wa Baraza la Madiwani

14.10.2017

MJI- KASALU.

YAH: TAARIFA YA KAMATI YA UCHUMI,ELIMU AFYA NA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JULAI-SEPTEMBER (2017/2018).

Katika kipindi cha mwezi Julai-Septemba **2017**,kamati ya Uchumi,Elimu Afya na Maji ilitekeleza shughuli zifuatazo kama zinavyoonekana kwenye hizi Idara zifuatazo.

- Idara ya Afya
- Idara ya Elimu Msingi
- Idara ya Elimu Sekondari
- Idara ya Maendeleo ya Jamii
- Idara ya Kilimo na Umwagiliaji
- Idara ya Mifugo na Uvuvi
- Idara ya Maji
- Utamaduni,Sanaa na Michezo
- Tasaf

Taarifa kamili imeambatanishwa.

Naomba kuwasilisha.

Mh.Gilbert Moshi

Mwenyekiti

Kamati ya Uchumi,Elimu Afya na Maji

Halmashauri ya Mji- KASULU

IDARA YA ELIMU MSINGI

Halmashauri ya Mji wa Kasulu ina jumla ya shule za Msingi 59 za serikali zenye jumla ya wanafunzi 55,322 kati yao wavulana 27448 na wasichana 27,874. Katika kipindi cha robo ya kwanza, 2017/2018 Idara ya Elimu Msingi imefanya kazi zifuatazo:-

- Kufanya vikao vya Kamati za shule za Mwilamvya na Mwibuye kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa na vyoo matundu 12.
- Kufuatilia ujenzi wa madarasa 6 na matundu ya vyoo 12 katika shule za Msingi Mwilamvya na Mwibuye. Kila shule ilipata mradi wa ujenzi wa madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo. Hali ya maendeleo ya ujenzi hadi sasa .
- Kutoa mafunzo kwa walimu 118 walimu wakuu 59 na waaratibu elimu kata 15 ya Umahiri wa kuhesabu darasa la I na II moduli ya 5-9
- Kufanya marekebisho ya taarifa za TSM na TSA kila kwenye mfumo BEMIS.
- Kuendelea kutoa huduma za kitaaluma na kitaalamu kwa wateja mbalimbali wanaofika ofisini.
- Kuendelea kusimamia utekelezaji wa sera ya “ELIMU BURE” kwa wanafunzi wote wa Elimu ya msingi.
- Kusimamia na kufuatailia usafi katika kituo cha Elimu maalum Kabanga.
- Kufanya maandalizi ya mwisho ya Mtihani wa Taifa wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2017 pamoja na kufanyika kwa mtihani huo. Maandalizi yaliyofanyika ni pamoja na:-
 - Kuandaa vikao vya kamati ya Uendeshaji Mitihani ngazi ya wilaya na Mkoa.
 - Kugawa baadhi ya vifaa muhimu kama vile vibao, rubber band na CAL.
 - Kufanya uteuzi wa wasimamizi wa Mtihani na kuwasilisha mkoani.
 - Kuchukua mtihani wa Taifa wa Kumaliza Elimu ya Msingi kutoka Mkoani kuja Halmashauri..
 - Kuandaa bajeti ya Mtihani.
 - Kuandaa malipo kwa wasimamizi.
 - Kufanya semina ya maelekezi kwa wasimamizi.
 - Kutawanya mitihani na wasimamizi katika vituo vya mitihani n.k.
- Kufanyika kwa Mtihani wa Taifa wa Kumaliza Elimu ya Msingi tarehe 06 – 07/09/2017. Taarifa ya watahiniwa ilikuwa kama ifuatavyo:-

WALIOSAJILIWA			WALIOFANYA MTIHANI			%	WASIOFANYA MTIHANI			%
WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML		WAV	WAS	JML	
1950	2293	4243	1942	2280	4222	99.5	8	13	21	0.5

- Kuhakiki watumishi hewa. Ni zoezi linalofanyika kila mwezi kwa kutumia Pay roll.
- Kuandaa taarifa ya LAAC ya Idara ya Elimu Msingi.
- Kukusanya madai mbalimbali ya watumishi walimu yasiyo mishahara.

- Kuendesha mafunzo kwa Walimu wakuu, walimu wa miradi shuleni wajumbe mmoja moja wa kamati za shule na Mfanyabiashara mmoja mmoja kutoka kila Mtaa. Mafunzo hayo yaliendeshwa na kuwezesha na Eguip-Tanzania.
- Kuhudhuria semina ya ugawaji wa vyandarua kwa wanafunzi wa darasa la I -III Mkoa wa Kigoma.
- Kuhamisha na kupokea wanafunzi wanaohama ndani na nje ya Halmashauri.
- Kukusanya takwimu za Walimu kwa majina yao toka kila shule. Zoezi hili lilifanyika hadi Agosti, 2017.
- Kutembelea shule ili kuona hali ya ufundishaji inavyoendelea Shule za Juhudi, Mwenge, Mwilamvya, Nyarumanga, Kanazi na Nyakabondo zimetembelewa.
- Kutembelea shule za Kiganamo, Bogwe, Kalema, Uhuru, Murubona na Umoja ili kuona hali ya utekelezaji wa Mtaala mpya ulioboreshwa.
- Kuhudhuria semina ya Early Grade Mathematics (EGM) iliyoyanyika Kigoma kuanzia Tarehe 1 – 5 /8/2017.
- Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa huduma za maji, Elimu Afya na usafi wa Mazingira shuleni kwa shule 88 za Msingi na sekondari.

IDARA YA ELIMU SEKONDARI

Idara ya Elimu Sekondari inasimamia shughuli za maendeleo katika Shule 25 za Sekondari, kati ya shule hizo, 11 ni za Serikali na 14 ni shule zisizo za serikali. Idara ina jumla ya walimu 299, Fundi sanifu Maabara 1 na maafisa 4. Idara imetekeleza majukumu yake kwa kipindi cha mwezi April – June, 2017 kwa kuzingatia Mpango Kazi wa Idara 2017/2018 kama ifuatavyo;

2. SHUGHULI NILIZOTEKELEZA

2.1 KUSHIRIKI UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA MTHANI YA KUHITIMU ELIMU YA MSINGI

Idara ya elimu sekondari ilishiriki kikamilifu katika usimamizi na uendeshaji wa Mthani wa Kumaliza Elimu ya Msingi PSLE 2017.

2.2 UHAKIKI MADENI YA WALIMU

Idara kwa kushirikiana na timu ya uhakiki wa madeni ya wilaya ilihakiki madeni ya walimu yasiyokuwa ya mishahara kuanzia julai 2016 hadi Juni 2017 na kuyawasilisha mamlaka za juu Mkoa na Wizara.

2.3 KUKUSANYA NA KUJAZA TAKWIMU MBALIMBALI ZA ELIMU KUTOKA SHULENI NA KUZIWASILISHA KATIKA MAMLAKA HUSIKA

Idara ilikusanya takwimu mabalimbali katika shule za sekondari na kuandaa taarifa mbalimbali kulingana na maelekezo na kuziwasilisha katika mamlaka husika

- Idadi ya wanafunzi, mikondo na walimu wanaofundisha kwa masomo.
- Taarifa za miradi ya ujenzi ya P4R.
- Kusahihisha taarifa za BEMIS.
- Taarifa za LAAC.
- Takwimu za watahiniwa wa kidato cha nne, maarifa na kidato cha pili.
- Uchambuzi wa matokeo ya Mithani ya Taifa.

2.4 KUFANYA MAANDALIZI YA MTHANI WA KIDATO CHA PILI NA CHA NNE MWAKA 2017

Idara imefanya maandalizi ya ufanyikaji wa mitihani ya kidato cha Pili (FTNA), Nne na Maarifa (CSEE & QT), 2017. Mitihani hii inatarajiwa kuanza kufanyika mwishoni mwa mwezi Oktoba na Novemba 2017.

2.5 KUSIMAMIA UENDESHAJI WA MTHANI YA UTIMILIFU WA KIDATO CHA NNE (MOCK) MKOA, NA PRE NATIONAL, 2017

Idara iliratibu maandalizi na ufanyikaji wa mitihani tajwa hapo juu yaani uandaaji wa bajeti, uteuzi wa walimu wa kutunga, kuhakiki, usimamizi wa ufanyikaji, usahihishaji na utoaji wa matokeo ya mtihani na matokeo yalikuwa kama kiambatisho kinavyoonesha. Mtihani wa Pre-National ulifanyika ili kuongeza mazoezi kwa watahiniwa wa shule za serikali na kuwa tayari katika ushindani kwa kufanya mitihani ambayo haikutungwa na walimu wanaofundisha masomo yao.

2.6 KUSIMAMIA UUNDWAJI WA ZA BODI ZA SHULE

Idara ilitoa maelekezo ya namna ya kupendekeza wajumbe wa Bodi za shule kwa shule zote za serikali na zisizo za serikali ambazo Bodi zao ziliisha muda wake ama zilikuwa hazina Bodi na kuhakikisha mapendekezo yote yamepelekwa katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Kigoma.

2.7 KUFANYA UFUATILJI WA USIMAMIZI WA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI

Kufanya ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji katika shule za sekondari na kutoa ushauri.

2.8 UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI KATIKA SHULE YA KIGOMA GRAND

Idara ilishiriki taratibu zote za maandalizi katika uwekaji wa jiwe la msingi katika shule ya KIGOMA GRAND tarehe 19 august, 2017. Jiwe la msingi liliwekwa na Mhe.Prof. Joyce Ndalichako (MB), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

2.9 KUENDESHA VIKAO MBALIMBALI VYA KIUTENDAJI

Idara iliendesha vikao kwa ajili ya uboreshaji wa utekelezaji wa majukumu ya kutoa elimu ya sekondari kwa wakuu wa shule za serikali na zisizo za serikali. Vikao hivyo ni kikao cha mrejesho wa

2.10 Kuhudhuria vikao vya Bodi za shule na kutoa ushauri wa changamoto mbalimbali

3.0 MAPOKEZI YA FEDHA

Idara ya Elimu Sekondari katika kipindi cha Robo ya Kwanza ya Julai– Septemba 2017/2018 Imepokea fedha Tsh. 73,201,775.09 na kutekeleza shughuli mbalimbali kwa mchangano ufuatao katika jedwali;

Na.	MUDA WA KAZI	SHUGHULI ILIYOFANYIKA	PESA ILIYOPOKELEWA
1.	Julai	Mgawo wa Elimu Bure	36,600,357.09
2	August	Mgawo wa Fedha za elimu bila malipo	36,601,424
3	Septemba		73,201,775.09

IDARA YA MAENDELEO YA JAMII

Taarifa ya idara ya maendeleo ya jamii ya robo ya kwanza. Katika taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo; Taarifa ya uhakiki wa asasi zisizo za kiserikali (NGOs) ,Taarifa ya mfuko wa wanawake (WDF), na Taarifa ya vikundi vilivyosajiliwa.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 katika robo ya kwanza, Halmashauri ya Mji wa Kasulu imefanikiwa kisajili vikundi 25 vya wanawake na vijana. Vikundi hivi vinajishughulisha na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kama vilivyoorodheshwa hapa chini:

Na	JINA LA KIKUNDI	NAMBA YA USAJILI	MAHALI KILIPO	TAREHE YA USAJILI	SHUGHULI ZA KIKUNDI
1	Chama cha madereva mchomoko	KTC /CBO/0099	MURUBON A	16.07.2015	Kusafirisha abiria ndani na nje ya mji wa kasulu
2	AMANI WOMEN	KTC /CBO/0103	KUMSENG A	22.07.2017	Kununua na kuuza mazao
3	NIYOKURU WAJANE WOMEN GROUP	KTC /CBO/0104	NYANSHA	30.7.2017	Kununua na kuuza mazao ya chakula pamoja na kilimo cha bustani.
4	KILOMBERO YOUTH GROUP	KTC /CBO/0106	MURUSI	12.8.2017	Kupakia mizigo ya mazao ya tumbaku
5	ILAKOZE GROUP WANAWAKE	KTC /CBO/0105	MURUSI	12.8.2017	Mazao ya chakula
6	TUPENDANE KWA SHAYO WANAWAKE	KTC /CBO/0107	MURUSI	16.8.2017	Kuweka na kukopa, kusaidiana katika shida na raha
7	NNUUR-ISLAMIC WOMEN GROUP	KTC /CBO/0109	MWILAVY A	16.8.2017	Kuweka na kukopa
8	KASULU TUMAINI HISA GROUP	KTC /CBO/0111	KUMSENG A	17.8.2017	Kuweka na kukopa
9	KASULU NEEMA GROUP	KTC /CBO/0110	KUMSENG A	17.8.2017	Kuweka na kukopa
10	TWENDE NA WAKATI WANAWAKE	KTC /CBO/0108	MURUFITI	21.8. 2017	Kutoa elimu ya ujasiliamali
11	JITEGEMEE VIKOBA	KTC /CBO/0112	HERU-JUU	19.8.2017	Kuweka na kukopa
12	UPATANISHO VIJANA GROUP	KTC /CBO/0113	MURUSI	21.8.2017	Uuzaji na ununuzi wa mazao
13	FURAHA WOMEN	KTC /CBO/0114	MURUSI	21.9.2017	Uuzaji wa duka la dawa muhimu
14	TUINUANE WALEMAVU GROUP	KTC /CBO/0115	NYANSHA	11.9.2017	Ufugaji wa nguruwe
15	KILIMO KWANZA WANAWAKE	KTC /CBO/0116	MURUSI	11.9.2017	Kilimo cha mihogo
16	EFSA WOMEN GROUP	KTC /CBO/0117	MURUSI	11.9.2017	Uuzaji wa chakula hotel
17	TUMAINI NYAKALELA	KTC /CBO/0118	HERU-JUU	11.9.2017	Ufugaji wa kuku wa kienyeji ujasiliamali kilimo cha mazao ya chakula
18	EDENI WOMEN	KTC	MURUSI	11.9.2017	Ununuzi na uuzaji

	GROUP	/CBO/0120			wa mazao
19	COMPLEX ACT YOUTH GROUP	KTC/CBO/012 1	MURUSI	11.09.2017	Sanaa ya uingizaji ,ufugaji wa kuku wa mayai
20	SAYUNI WOMEN GROUP	KTC/CBO/012 2	MURUSI	11.09.2017	Kuuza na kununua mazao ya chakula
21	ZANTEL YOUTH GROUP	KTC/CBO/012 3	NYUMBIG WA	12.09.2017	Kilimo cha matunda
22	MAANDARIO WOMEN	KTC/CBO/012 4	MURUSI	26.29. 2017	Kuuza na kununua mazao ya chakula.
23	VIJANA WAFUGA BATA	KTC/CBO/012 5	MWILAVY A	28.09.2017	Ufugaji bata.
24	JITIHADA WOMEN GROUP	KTC/CBO/012 6	KUMSENG A	14.03.2017	Kuweka na kukopa na kilimo cha chakulaovyamaji.
25	SHALOOM WOMEN GROUP	KTC/CBO/012 7	MURUSI	29.09.2017	Uuzaji wa mbegu na mboleafirishaabirian amizigoyao.

MASHIRIKA YA SIYO KUWA YA KISERIKALI (NGOs) YALIYO HAKIKIWA NAKUTAMBULIWA KUFANYAKAZI KATIKA HALMASHAURI YA MJI WA KASULU .

Katika Halmashauri ya mji wa Kasulu kuna mashirika 15 yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanayotambuliwa na Idara ya Maendeleo ya Jamii. Mashirika haya yanatoa huduma zake ndani na nje ya mipaka ya Halmashauri ya mji wa Kasulu. Baadhi ya mashirika haya yanatoa huduma zake kwa wakimbizi. Aidha mashirika yanayotolewa taarifa zake ni yale ambayo walileta utambulisho na yamekuwa yakileta taarifa zao za utekelezaji. Mashirika hayo yameorodheshwa hapa chini.

TAARIFA YA NGOs ZINAZOFANYAKAZI KATIKA HALMASHAURI YA MJI.

	JINA LA NGOs	MAHALI ILIPO/ENEO LA OFISI	KAZI /SHUGHILI ZA NGOs	NAMBA ZA NGOs	MWAKA WA WAKUANZA
1	WESTERN TANGANYIKA ENTERPRENEUR IN AGRICULTURE REBAND FISH CAPTIVITY ORGANIZATION (WETAAIFICO)	MKOA WA KIGOMA , WILAYA YA KASULU, MTA A WA MRUSI	KUJENGA UJUZI WA VITENDO KATIKA KILIMO , UFUGAJI WA WANYAMA NA SAMAKI. UFUGAJI WA NYUKI NA USINDIKAJI WA CHAKULA (NK)	OONGOs/ 00004592	15/07/2010
2	CONSORTIUM	KASULU TC MURUSI	KUTUNZA MAZINGIRA ,KUWAPATIA	No S. A 17243	24 TH JANUARY, 2011

			ELIMU YA KIAFYA KWA JAMII		
3	SAVE FOR DEVELOPMENT AND RELIEF ASSOCIATION(SADERA)	KASULU TC KIGANAMO	KUTOA ELIMU YA AFYA KWA JAMII YA KASULU MJINI NA VIJINI. KU WEZESHA VIKUNDI VYA WA NAWAKE NA VIJANA WA KIKE NA KIUME KIUCHUMI.	00NGOs/00001461	12/03/2012
4	TREECOVER FOUNDATION (TCF)	KASULU TC BARABARA YA KIBONDO MKABARA NA OFISI YA HALMASHAUR YA MJI.	UTUNZAJI WA MAZINGIRA PAMOJA NA KUANDAA VITARU VYA MITI.	OONGOs/0009245	29 TH MAY 2017
5	WAKWANZA PARALEGAL ORGANIZATION (WAPAO)	KASULU TC MURUSI	KUELIMISHA JAMII JUU YA MASUALA KISHERIA NA HAKI ZA KIJAMII PAMOJA NA KUSURUHISHA MIGOGORO YA KIJAMII.	06/NGOs/08451.	
6	HAKI ORGANIZATION	KASULU TC MTAA WAMMISSION AGRICANA	KUTOA HUDUMA ZA KISHERIA KWA WTOTO WA MITAANI, MITAA, WAJANE NA MAYATIMA.	SO. NO. 11963	11 TH AUGUST 2003
7	TANZANIA AGRICULTURE AND ENVIRONMENT DEVELOPMENT ORGANIZATION, (T.A.E.D.O)	KASULU T.C MRUVUMU	KUTUNZA MAZINGIRA, KUO TESHAJI WA MITI NA UPANDAJI MITI PAMOJA NA KILIMO CHA MSETO KWA KUTUMIA MITI INAYORUTUBISHA ARTHI NA MBOLEA YA SAMADI NA MBOJI	SO.14983.	2 AUGUST 2004

8	TANZANIA RURAL DEVELOPMENT AND RELIEF ORGANIZATION (TARUDERO)	KASULU TC T.T.C	KUTOA HUDUMA KUSAIDIA WANAWAKE NA VIJANA PAMOJA NA WAKIMBIZI WALIO ATHIRIKA KIJAMII HASA WALE WALIO MAKAMBINI	SO NO 11470	
9	FIGHTERS FOR DEVELOPMENT SUSTAINABILITY (FIDESU)		UTUNZAJI WA MAZINGIRA ,UOTESHAJI WA MICHE YA MITI, AFYA , KILIMO, UFUGAJI WA NYUKI , UFUGAJI WA SAMAKI,KUKU, NA KILIMO CHAMIWA NA MIHOGO.	OONGO/08593	16 TH MAY 2016
10	KASULU MOBILE EYE CARE FOUNDATION(KAMECAF)	KASULU T.C KWIZERA	KUELIMISHA JAMII KUHUSU MAGONJWA YA MACHO NA KUTOA MATIBABU YAKE.	00NGO/0008800	25 TH OCTOBER/2016
11	DISABILITY RELIEF SERVICES (DRS)-TANZANIA	KASULU TC MATAA WA KWIZERA	KUTOA HUDUMU ZA VIWEZESHA (SUPPORTING GEAR) KWA WATU WENYE ULEMAVU KASULU MJINI NA VIJINI ILI KUWALAHISHIA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAO YA KIMAISHA. KUWAJENGEA		January 2016
12	BENEVOLENT INSTITUTE OF DEVELOPMENT INITIATIVE	KASULU T.C MATAA WA NYASHA	KUTOA MAFUNZO KWA WAKULIMA NA JUU YA MIFUNGO,KUHUSU UFUNGAJI	SO. 12676	AUGUST 2004

	IN TANZANIA,(BIDII-TANZANIA)		BORA WA NGOMBE WA MAZIWA NA NYAMA YA NGURUWE,MBUZ I NA KUKU , NA PAMOJA NA KILIMO BORA CHA MAZAO YA CHAKULA ,		
13	KASULU HEALTH HOME BASED CARE ORGANIZATION (KAHHOBACO)	KASULU T.C MTA A WA NYASHA	CLINIC YA AFYAYA UZAZI NA MTOTO PAMOJA NA KUTOA ELIMU YA JAMII JUU YA KUZUIA MAGONJWA MBALI MBALI KAMA VILE MALARIA NA HIV/AIDS	OO NGO/00003052	08 TH APRIL 2009
14	TANZANIA HELP ELDERLY AND SINGLE PARENT ORGANIZATION (THESPO)	KASULU T.C JIRANI NA KANISA KUU LA ANGLICANA	KUSAIDIA WATOTO WANA OISHI KATIKA MAZINGIRA HATARISHI PAMOJA NA KUSAIDIA YATIMA , WAJANE NA WAZEE. KUTOA ELIMU KWA JAMII KUHUSIANA NA MAGONJWA MBALI MBALI IKIWEMO MAGONJWA YA MLIPUKO PAMOJA NA MAZINGIRA.	00NGO/00007863	5 TH MARCH 2015
15	SAIDIA WAZEE (SAWATA)	KASULU T.C UJENZI	KUTOA HUDUMA ZA KUSAIDIA WAZEE KWA AJILI YA KUINUA MAISHA YAO NA KUPUNGO MISONGO YA WAZEENI	SO.NO .8039	16/10/2008

16	AMENITY NON PROFIT CHARITY ORGANIZAT ION (ANCO)	KASULU T.C MURUBONA MTAA WA UMOJA	UWEZESHAJI WANAWAKE KIJAMII NA KIUCHUMI PAMOJA NA ILINZI WA HAKI NA USTAWI WA WATOTO	O6NGO/0 0005896	19 TH OCTOBER 2012
----	----------------------------------------------------------------	--------------------------------------------	-----------------------------------------------------------------------------------------------------------	--------------------	----------------------------------

MAPENDEKEZO YA VIKUNDI VINAVYOTEGEMEWA KUPATA MIKOPO

s/n	Jina la kikundi	Kata	kiasi	Mradi wa kikundi
1.	Bwiza women	Murusi	2,000,000	Ufugaji wa kuku
2.	Tupendane women Kwa Shayo group	Murusi	2,000,000	Uuzaji wa mazao
3.	Tuinue walemavu group	Nyansha	2,500,000	Ufugaji wa nguruwe
4.	Tuhudumiane wajane	Nyansha	3,000,000	Kilimo cha bustani ,kuweka na kukopa
5	Itangigomba women	Kumsenga	3,000,000	Ununuzi na uuzaji wa mazao
6	Furaha women	Murusi	3,000,000	Duka la dawa baridi
7	Kayore youth	Murubona	3,000,000	Mradi wa kutengeneza viatu
8	Mshikamano women	Murubona	4,000,000	Kutengeneza sabuni za maji na masweta
9	Amani women	Kumsenga	2,000,000	Kulangua mazao na kuuza
10	Niyonkuru wajane	Murubona	2,500,000	Kununua na kuuza mazao
	Jumla		27,000,000	

IDARA YA KILIMO NA UMWAGILIAJI

Idara ya Kilimo Umwagiliaji na Ushirika Mji ina jumla ya watumishi 12,kati ya hao watumishi 2 wako ngazi ya ofisi kuu na 10 ngazi ya kata na mtaa.Katika kipindi cha robo ya kwanza cha mwaka wa fedha 2017/18 katika kipindi hiki idara ilitekeleza shughuli kusimamia na kufuatilia ujenzi wa soko la sofya .paomoja na shughuli za ugani kama zilivyoainishwa hapa chini.

HALI YA HEWA.

Katika Kipindi cha robo ya kwanza kimekuwa cha kiangazi ambacho wakulima walikitumia kuzalisha mazao ya bustani hasa mboga za majani ,mahindi na maharage maeneo ya bondeni yenye ardhi oevu.

PEMBEJEO ZA KILIMO

Mwaka huu wa fedha 2017/18 serikali haitatoa ruzuku za pembejeo kwa mfumo wa vocha kama ilivyofanyika kwa miaka ya nyuma badala yake serikali imeelekeza wakala wa pembejeo kutoa bei elekezi kwa mbolea ya kupandia aina ya DAP kuwa itauzwa kwa sh.56,000 badala ya sh 65,000 inayouzwa na wafanyabiashara katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu na Urea Kuuzwa kwa sh 43,679 badala y ash.48,000 iliyopo madukani sasa.

4.SHUGHULI ZA UGANI.

Katika msimu wa Kilimo 2017/18 idara ya kilimo imepanga kutekeleza shughuliza

Kwa kuzingatia malengo yafuatayo:-

MALENGO YA KILIMO MSIMU 2017/18

ZAO	LENGO(HEKTA)	UVUNAJI TANI
MAHINDI	30,000	52,500
JUMLA NDOGO	30,000	52,500
MAHARAGE	5950	29,750
MBAAZI	105	105
NJEGERE	12.5	12.5
JUMLA NDOGO	6067.5	2,929
MIHOGO	8960	89,600
VIAZI VITAMU	399	3,192

VIAZI MVIRINGO	70	595
MAGIMBI	18	180
JUMLA NDOGO	9,447	93,567
VITUNGUU SAUMU	10	75
TANGAWIZI	9	90
JUMLA NDOGO	19	165
NYANYA	90	2250
VITUNGUU	62	465
HOHO	28	28
KABICHI	38	760
MCHICHA	21	21
CHINESE KABICHI	7	7
KAROTI	5	20
NYANYA CHUNGU	14	72
MATANGO	6	24
TIKITI	8	80
JUMLA NDOGO	269	3,727
KAHAWA	20	13
ALIZETI	35	-
KARANGA	95	95
NDIZI MBIVU	37	225
NDIZI MBICHICHI	98	450
MIWA	59	590
JUMLA	361	1,360

MALIMAO	12	12
MACHUNGWA	16	32
CHENZA	6	12
AVOCARDO	5	50
PAPAI	12	120
PASHENI	5	5
JUMLA NDOGO	56	231
JUMLA KUU	46,219	154,479

IDARA YA MAJI

TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA IDARA YA MAJI KWA ROBO YA KWANZA

Katika Robo hii ya kwanza Idara ya Maji iliendelea kusimamia ujenzi wa miradi ya maji Kimobwa, Heru juu na Muhunga. Utekelezaji wa miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali ambapo mradi wa maji Heru juu umekamilika kwa **75%**, Mradi wa Maji kimobwa umekamilika kwa **79%** na Mradi wa maji Muhunga umekamilika kwa **70%**. Wakazi katika miradi ya maeneo yote matatu wameanza kunufaika na huduma ya maji kupitia miradi hiyo. Hata hivyo miradi hiyo ilitarajia kukamilika tarehe **09/11/2017** kama fedha ingekuwa kwa wakati. Mpaka kufikia hatua hiyo mkandarasi alikuwa amelipwa asilimia **15** ya fedha zote za utekelezaji wa mradi. Mkandarasi katika miradi ya Heru-Juu na Kimobwa ameomba kuongezewa muda wa mwezi mmoja kwani fedha ya miradi hiyo imengia tarehe **02.11.2017** na mkandarasi wa mradi wa Muhunga ameomba kuongezewa miezi **2** kwasababu anatakiwa kujenga tenki la Maji ambalo litatakiwa kukaa na maji kwa **siku 21** kabla ya kufunikwa.

Vilevile katika Robo hii Idara ya Maji iliendeleza zoezi la kuunda na kusajili vyombo vya Watumia maji. Vyombo vya watumia Maji vimeundwa katika maeneo ya Kanazi, Ruhita, Heru juu, Mwanga B, Nyumbigwa, Kabanga na Msambara. Utaratibu wa kuvisajili umekamilika kwa maeneo ya kabanga na Msambara. Usajili kwa maeneo yaliyobakia umekamilishwa katika Robo ya pili ya mwaka **2017/18**.

Changamoto kubwa zinazokabili Idara ya maji hivi sasa ni uzalishaji wa maji mdogo kuliko mahitaji ya maji kwa Wakazi wa Halmashauri ya mji wa Kasulu. Wakazi wanaopata huduma ya maji ni **58%**. Katika kukabiliana na Changamoto hili, Mipango ya utekelezaji wa Miradi umeandaliwa na utekelezaji wake umepangwa kufanyika kwa kipindi cha miaka mitano kati ya

2016 -2021. Ujenzi wa miradi ya maji inayoendelea katika maeneo ya kimobwa, Heru juu na Muhunga ni sehemu ya utekelezaji wa mpango hiyo.

Changamoto ingine ni Uhaba wa Watumishi katika sekta ya Maji. Idara ina watumishi **4** ambao ni waajiriwa ikilinganishwa na mahitaji halisi ya watumishi **21**. Upungufu huo wa jumla ya watumishi 17 unapunguza kasi na ufanisi katika utoaji wa huduma ya Maji. Maombi kuonesha hitaji la watumishi wapya yamewasilishwa TAMISEMI na ufuatiliaji unaendelea.

TAARIFA YA ROBO YA KWANZA YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI KASULU.

1.0 KAZI ZILIZOPANGWA NA KUTEKELEZWA

Katika kipindi cha robo ya Kwanza kazi zilizotekelezwa ni hizi zifuatazo:-

- Wateja wameunganishiwa huduma ya maji ukiinganisha na uzalishaji
- Ugawaji wa maji, kutibu maji na kufanya usafi wa vyanzo
- Upimaji wa unadhifu na ubora wa maji katika vyanzo vya maji na vituo vya kutekea maji.
- Jumla ya mivujo 123 imebainiwa na 114 imedhibitiwa sawa na 92. 7%
- Usomaji wa dira umefanyika na jumla ya madai 8,827 yenye thamani ya Tshs 46,014,936.20 yameandaliwa na kusambazwa kwa wateja.
- Usimamaizi wa kina na wa karibu wa mradi wa maji wa Kimobwa umefanyika. Kazi ya uchimbaji wa mitaro ya bomba za kutawanya maji imefanyika ikiwa ni pamoja na ufungaji wa mabomba km 1.2.
- Kufanya matengenezo ya dharura yaliyosababishwa na uchongaji wa barabara.
- Kusikiliza matatizo ya wateja na kuyatutua
- Kufanya shughuli za usimamizi wa mapato ya Mamlaka

2.0. CHANGAMOTO

Zifuatazo ni baadhi ya changamoto zinazoathiri upatikanaji wa huduma ya maji mjini

- Kutokuwa na dira za kutosha kwa ajili ya kudhibiti upotevu wa maji
- Kutokuwa na mtambo wa kusafisha maji.
- Wateja wa kawaida na taasisi za serikali kutolipia Ankara zao kwa wakati.
- Miundombinu ya mabomba kuharibiwa kwa kiasi kikubwa wakati wa uchongaji wa barabara.

3.0. UTATUZI WA CHANGAMOTO

Mamlaka imeanza kutatua baadhi ya changamoto zilizopo kama ifuatavyo.

- Ufuatiliaji wa madeni umefanyika ili kupata mapato ya kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa Mamlaka.

- Mamlaka kwenye bajeti yake ya mwaka 2017/2018 imepanga kununua dira za maji 500 na kuzifunga ili kudhibiti upotevu wa maji na vilevile mivuho imedhibitiwa kila ilipojitokeza.
- Mamlaka imeongeza chanzo kingine cha maji cha mto Chai na kupanua mtandao wa maji

KITENGO CHA UTAMADUNI NA MICHEZO

UTAMADUNI NA SANAA:-

- i. Kushauri na kuelekeza taratibu za Usajili wa Vikundi vya Sanaa, Wasanii binafsi, kazi za Sanaa na utengenezaji wa Katiba na Wasifu wa msanii binafsi. Jumla ya wasanii binafsi wane (4) walishauliwa ambao ni Bethuel Johnson, Shaid A.Bukambu, Amani Issa Ndigeze na Daniel Elias na Kikundi kimoja ni Sunrise Arts Group.
- ii. Kutangaza maeneo ya Kihistoria (Minara miwili ya Uhuru, Jengo la Mjerumani – DC, Eneo la makazi na makaburi ya Mwami Gwasa na Ntare.
- iii. Kupokea wageni wa SIDO kutoka Kigoma waliokitembelea Kikundi cha **Kasulu Theatre Art Group**, kwa ajiri ya shughuli za maonyesho katika Halmashauri yetu ya Kasulu Mji.
- iv. Kutoa Vibali vya kucheza Disco, Dansi na Show. Kutoa Vibali vya Matangazo ya shughuli za kibiashara kwa kutumia vipaza sauti.

2. MICHEZO

- 1) Kushirikiana na Vilabu vya Kasulu United na Red Star kwa ajili ya maandalizi ya kushiriki katika Ligi Daraja la III Mkoa.
- 2) Kushirikiana na Chama cha Kareti, kuandaa Rasmu ya Katiba ya Chama hicho katika Halmashauri ya Mji Kasulu.
- 3) Kukutana na Walimu wa Michezo kwa lengo la kuwahamasisha ili washiriki Mafunzo ya mpira wa Miguu na Mpira Pete hapahapa kasulu.
- 4) Kuendesha mafunzo ya mpira ya miguu chini ya mkufunzi Logasian Kaijage Mkufunzi wa FIFA aliyeteuliwa na chama cha mpira Nchini TFF.
- 5) Kuandaa timu ya mpira wa miguu kwa ajiri ya mashindano ya ujirani mwana na Nchi ya BURUNDI.
- 6) Kufanya kikao na Wadau wa michezo. Ili kupanga mikakati ya kuendeleza michezo katika Halmashauri ya Mji Kasulu.
- 7) Kwa kushirikiana na wadau wa michezo kuweka mikakati ya kuinua michezo katika Halmashauri ya Mji ili michezo ichezwe kwa rika zote katika jamii.
- 8) Kuratibu mazoezi ya kila wiki ya pili ya mwezi kama agizo la Makamu wa Rais linavyoagiza.
- 9) Kuhudhuria kikao cha maafisa Michezo Kigoma kwa ajiri ya maandalizi ya ligi ya ujirani mwema.

2. VIJANA:-

- a) Kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii kuratibu mchakato wa kuanzisha SACCOS ya Vijana inayitwa “TUUNGANE VIJANA SACCOS (TUVISA).
- b) Kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii kuandaa mapendekezo ya Vikundi vya Vijana, vilivyokidhi vigezo vya kupewa Mkopo na Halmashauri ya Mji.
- c) Kuandaa taarifa za Maendeleo ya Vijana.
- d) Kuendelea na ufuatiliaji wa kujua vikundi hai vya Vijana ili kuwa na Orodha sahihi.

2. MATARAJIO.

- Halmashauri ya Mji kutenga fedha za kuendesha utamaduni na michezo.
- Kujenga kiwanja cha michezo cha Halmashauri ya Mji.
- Kuendesha mabonanza na tamasha za sanaa na michezo kwa lengo la kuibua na kuendeleza vipaji.
- Kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa makocha, waamuzi na walimu wa sanaa.
- Kuhamasisha makampuni/mashirika Taasisi na watu binafsi kuwekeza katika michezo na sanaa.

TAARIFA YA SHUGHULI ZA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI KIPINDI

CHA JULAI – SEPTEMBER 2017

1.0 Utangulizi

Taarifa utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini inajumusha shughuli zilizo tekelezwa katika kipindi cha Julai – Septemba 2017 ambapo uhawilishaji fedha dilisha la malipo Julai – Agosti 2017 ilikuwa miongoni mwa shughuli kuu zilizotekelezwa. Ikiwa ni dilisha la malipo la awamu ya kumi na tatu (13) kaya zipatazo 4,837 (98.7%) kati ya kaya 4,903 zilihawilishiwa fedha za ruzuku. Kaya 66 (1.3%) hazikupokea malipo kutokana na kutotoke katika vituo vya malipo na vifo kwa kaya zilizokuwa mwanakaya mmoja.

2.0 Usimamizi na ufuatiliaji

Katika kipindi cha Julai – Septemba 2017, shughuli za Mpango zilisimamiwa, kufuatiliwa na watendaji kutoka Halmashauri ya mji wakiwemo Mkurugenzi wa Mji, Mweka Hazina, Mratibu wa Mpango, Mhasibu wa Mpango, Afisa Ufuatiliaji (mwajiliwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii), Mkaguzi wa ndani, wawezeshaji, watendaji wa mitaa na Maafisa wa jeshi la polisi. Wote hawa walitekeleza wajibu wao ili kuhakikisha shughuli zinatekelezwa kwa kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa.

2.1 Uandaaji wa Taarifa

Hata hivyo taarifa za utekelezaji wa shughuli ziliandaliwa na kuwasilishwa katika mamlaka na ngazi husika zilizopaswa kuwasilishwa taarifa. Taarifa za malipo ya Julai – Agosti 2017 zilizo paswa kuingizwa kwenye mifumo ya utoaji taarifa ziliandaliwa na kuingizwa kwenye mifumo ya MIS na OPSYS.

3.0 Taarifa za fedha

3.1 Fedha pokelewa

Halmashari ya Mji Kasulu katika kipindi cha Julai – Septemba 2017 ilipokea fedha kutoka TASAF makao makuu TZS. **318,917,440.00** kwa ajiri ya uhawilishaji malipo ya mwezi Julai – Augosti na Septemba - Oktoba, 2017. Rejea jedwali Na.1

Jedwali Na. 1: Fedha pokelewa za Uhawilishaji Julai - Septemba 2017

S/N	Lengo / Shughuli	Fedha pokelewa katika Robo hii ya Julai – Sept. 2017	Fedha za Uhawilishaji zilizo pokelewa robo zilizopita	Limbikizo la Fedha pokelewa tangu kuzinduliwa kwa Mpango
1.	Fedha pokelewa robo zilizopita	0	2,442,019,219.61	2,442,019,219.61
2.	Uhawilishaji Julai-Aug. 2017	155,170,720.00	0	155,170,720.00
3.	Uhawilishaji Sept.-Okt. 2017	163,746,720.00	0	163,746,720.00
4.	Jumla	318,917,440.00	2,442,019,219.61	2,760,936,659.61

3.2 Fedha tumika

Katika kipindi cha Julai - Septemba 2017 Halmashari imetumia TZS 151,322,720.00 kwa uhawilishaji wa fedha dilisha la malipo ya mwezi Julai - August 2017, kiasi cha TZS 1,648,000.00 fedha za walengwa 66 ambao hawakupokea malipo zilirejeshwa TASAF makao makuu. Rejea Jedwali Na. 2

Fedha zilizo pokelewa kwa malipo ya Septemba – Oktoba TSZ 163,746,720.00 zitatumika katika robo ya Oktoba – Desemba 2017.

Jedwali Na. 2: Fedha za uhawilishaji zilizotumika Julai - Septemba 2017

S/N	Lengo / Shughuli	Fedha tumika katika robo hii ya Julai – Septemba 2017	Fedha tumika katika robo zilizopita tangu kuzinduliwa kwa Mpango.	Limbikizo la Fedha tumika tangu kuzinduliwa kwa Mpango
1.	Fesha rejeshwa TASAF Julai - Aug. 2017	1,648,000.00	55,825,665.00	57,473,665.00
2.	Matumizi ya Robo hii Julai – Septemba 2017	151,322,720.00	2,386,193,554.61	2,537,516,274.61
Jumla ya fedha tumika Julai - Augosti 2017		152,970,720.00	2,442,019,219.61	2,594,989,939.61

4.0 Changamoto

- i. Mabadiliko ya kanuni za ukokotoaji wa fedha za usimamimizi na ufuatiliaji wa shughuli za mpango dhidi ya ukokotoaji wa awali wa 8.5%, 1% na 1.5% kwa ngazi za mamlaka ya utekelezaji emepelekea ugumu wa utekelezaji wa shughuli za mpango ndani ya mamlaka ya utekelezaji.
- ii. Maboresho ya yanayoratibiwa na TASAF makao makuu juu ya mufumo wa uingizaji wa taarifa za mpango MIS yaripelekea ucheleweshwaji wa shughuli zilizo paswa kutekelezwa.

4.1 Utatuzi wa changamoto / matazamio ya mbele

- i. Halmashuri ilipendekeza kwa TASAF Makao makuu kupitia upya kanuni za ukokotoaji wa fedha za usimamimizi na ufuatiliaji wa shughuli za mpango.
- ii. Mawasiliano kati ya Halmashuri na TASAF Makao makuu yalifanyika ili kupata utatuzi wa changamoto za mfumo wa uingizaji taarifa za mpango MIS na utatuzi wa changamoto hii ulipatikana.

5.0 Hitimisho

Pamoja na changamoto, shughuli za mpango hususani uhawilishaji fedha malipo ya Julai – Augosti 2017 zilitekelezwa kama zilivyo pangwa. Viambatisho mbalimbali vimeambatishwa ili kutoa ufafanuzi wa kina wa taarifa hii.

IDARA YA AFYA

Mheshimiwa Mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Uchumi, Afya na Maji, ifuatayo ni taarifa ya utendaji kazi wa Idara Afya kwa kipindi cha Julai – Sept 2017.

Utangulizi

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imebeba utendaji wa kazi sehemu kuu tatu za Idara ya Afya ambazo ni Afya Kinga, tiba na shughuli za utawala.

1. Shughuli za Afya Kinga

Uelimishaji wa jamii

Elimu ya Afya kwa Jamii juu ya kujikinga na Magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza ilitolewa kwa wateja wote waliofika katika vituo vya kutolea huduma za Afya.

Upimaji wa makuzi ya watoto

Mahudhurio ya watoto chini ya Mwaka mmoja (<1 YR) ilikuwa ni watoto 14521 ambapo **wakiume** walikuwa 7084 na **wakike** walikuwa 7437. **Utapiamlo mkali** ulikuwa kwa watoto wa **kiume 20** na **30**

kwa watoto wa **kike**. Utapiamlo wa **wastani** kwa watoto wa **kiume** ulikuwa 521 na 580 kwa watoto wa **kike**. Hali **nzuri ya lishe** ilikuwa ni 6483 kwa watoto wa **kiume na 6730** kwa watoto wa **kike**

Mahudhurio ya watoto chini ya miaka mitano ilikuwa 29009 ambapo watoto wa kiume **ilikuwa 14808** na watoto wa kike **walikuwa 14201**. Hali ya utapiamlo mkali kwa watoto wa kiume ilikuwa 63 na wakike ilikuwa 98. Utapiamlo wa wastani kwa watoto wa kiume 1536 na 1863 kwa watoto wa kike. Hali nzuri ya lishe ilikuwa 12633 kwa watoto wa kiume na 12180 kwa watoto wa kike.

Chanjo:

Watoto 14,366 walifika kupata chanjo ya kuzuia magonjwa yanayoweza kuzuiwa kwa chanjo kwa kipindi cha mwezi Julai –Sept 2017.

Na	Aina ya chanjo	Lengo	Waliopata chanjo	Asilimia
1	Chanjo dhidi ya kifua kikuu	2040	3385	165
2	Chanjo dhidi ya Polio(O)	2040	1782	87
3	Chanjo ya polio 3	2040	1887	92
4	Chanjo dhidi ya homa ya ini(pecv)	2040	1933	94
5	Chanjo dhidi ya surua rubella(1)	2040	1632	80
6	Chanjo dhidi ya sura rubella(2)	2040	1928	94
7	Chanjo dhidi ya kichomi(penta)	2040	1782	87
8	ROTA(KUHARISHA)	2040	1928	94
9	T.T 2+ (pepo punda)	2040	1782	87
10	VITAMINI A	2040	1923	94

Idadi ya watu wanaochanjwa inakuwa kubwa zaidi kwa sababu ya huduma kupatikana katika eneo linalokusudiwa na kituo cha kliniki ya baba, mama na mtoto.

Uzazi wa mpango

Jumla ya wateja 3730 walifika kwa huduma ya uzazi wa mpango kwa mara ya kwanza, na wakati wateja 379 walikuja kwa marudio ya pili au zaidi.

UZUIAJI WA MAGONJWA YA KUAMBUKIZA.

Jumla ya taarifa za kila Wiki 48 za magonjwa ya kuambukiza yanayotolewa Taarifa Kitaifa na Kimataifa (IDWE) zilikusanywa na kutumwa mkoani kila siku ya Alhamisi ya wiki

2. Taarifa ya Tiba

>Utendaji kazi sehemu ya wagonjwa wa nje (OPD)

>Mahudhurio

Katika vituo vya kutolea huduma za Afya katika halmashauri ya mji mwezi Julai – Sept 2017 vilipokea jumla ya wateja 26,950 waliohudhuria kupatiwa huduma za Afya kama ifuatavyo.

Jedwali ii :- Mahudhurio

Mahudhurio ya Nje (OPD)

Chini ya miaka 5		Zaidi ya miaka 5				Msamaha/miaka 60 na zaidi		Jumla
M	F	M	F			M	F	
3861	3729	5171	8946			890	1637	24234
7590		14117				2527		24234

iii -Mahudhurio ya marudio (OPD REATENDANCE)

chini ya miaka 5		zaidi ya miaka 5				Msamaha/miaka 60 na zaidi		Jumla
M	F	M	F			M	F	
378	475	695	861			166	201	2716
793		1556				367		2716

TIBA KWA WAZEE WENYE UMRI WA MIAKA 60 NA KUENDELEA

MAHUDHURIO YA KWANZA		MARUDIO	
M	F	M	F
57	110	166	201
167		367	

Hali ya magonjwa katika mwezi Julai-Sept 2017

Hali ya magonjwa sehemu ya tiba ya wagonjwa wa nje (OPD) Ugonjwa wa Malaria uliendelea kuisumbua jamii ya Kasulu kama ilivyo kuwa miezi mingine.

Hali ya magonjwa kumi yaliyoisumbua jamii zaidi imeoneshwa katika jedwali VIII. Magonjwa muhimu katika mwezi Julai -Sept 2017.

Na	Aina ya ugonjwa kwa watoto chini ya miaka 5	Idadi	%
1	Magonjwa ya njia ya hewa	1350	29
2	Malaria	1294	28
3	Magonjwa ya kuhara	635	13
4	Magonjwa ya njia ya mkojo	600	13
5	GIT	228	4
6	kichomi	174	3
7	Magonjwa ya Ngozi	120	2
8	Magonjwa mengineyo	62	1
9	Magonjwa ya masikio	60	1
10	Magonjwa ya macho	47	1
JUMLA		4570	93

Jedwali I IX: Magonjwa kumi yaliyoongoza kusumbua watu wenye umri zaidi ya miaka 5.

Na	Aina ya ugonjwa kwa watu wenye umri zaidi ya miaka 5	Idadi	%
1	Magonjwa ya njia ya mkojo	2806	21
2	Malaria	2692	20
3	Magonjwa ya njia ya hewa	2636	20
4	Minyoo	1839	14
5	Magonjwa ya matatizo ya meno	928	7
6	Magonjwa ya kuhara	611	4
7	GIT	500	3
8	kifafa	400	3

9	Matatizo ya kujifungua	369	2
10	Upasuaji	342	2
JUMLA		13123	96

WODI YA WAZAZI

Halmashauri ya mji kasulu ilikuwa na akina mama 2349 waliojifungua katika mwezi Julai-Sept 2017. Kati yao akina mama 2118 walijifungua kwa njia ya kawaida, wakati 253 walijifungua kwa njia ya upasuaji. Watoto 43 walizaliwa wafu.

VIFO

Kulikuwa na vifo 96 vya wagonjwa waliokuwa wamekuja kupata matibabu na Sababu kubwa ya vifo ilikuwa ni Kama ifuatavyo:-

Vifo vya watoto chini ya miaka mitano =20			Vifo vya wagonjwa zaidi ya miaka 5=76		
Na	Aina ya ugonjwa	Idadi ya vifo	Na	Aina ya ugonjwa	Idadi ya vifo
1	Malaria	7	1	malaria	19
2	Respiratory distress	6	2	Magonjwa ya kupungukiwa maji mwilini	7
3	Magonjwa ya moyo	3	3	Magonjwa ya moyo	32
4	Ajali	2	6	Magonjwa njia ya hewa	7
5	Magonjwa ya kupungukiwa maji mwilini	1	7	Kreptococo HIV	5
6	Septicaemia	1	8	Magonjwa ya kuhara	6
	JUMLA	20		JUMLA	76

Shughuli za upasuaji

Jumla ya wagonjwa 84 walifanyiwa upasuaji mkubwa wakati Wagonjwa 1342 walifanyiwa upasuaji mdogo. Jumla kulikuwa na upasuaji 1426.

Shughuli za X ray

Jumla ya wagonjwa 278 walifanyiwa uchunguzi wa mionzi kwa mwezi Julai –Sept 2017.

Shughuli za TB na UKOMA

Wagonjwa 30 walikuja kupata huduma za kifua kikuu na Ukoma walikuwa 0 .

Shughuli za uchunguzi

Uchunguzi kwa njia ya mionzi na maabara hufanyika kwa wagonjwa wote kwa mujibu wa maagizo ya madaktari. Upande wa maabara shughuli zilizotekelezwa kama ifuatavyo:-

Aina ya kipimo	Jumla	Idadi chanya (+ve)	Maelezo
Vipimo vya damu (Malaria)	6254	677	Kuwa na vimelea vya Malaria
Vipimo vya wekundu wa damu	1975	241	HB kuwa chini ya 70g/L(50%)
Vipimo vya kaswende	81	0	
Vipimo vya choo	378	42	Choo kubwa kuwa na vijidudu vya minyoo ya safura ,ascaries,E. Histolytica
Vipimo vya makohozi	125	7	Vipimo vya makohozi kuwa na vimelea vya kifua kikuu
Vipimo vya mkojo	1531	42	Wingi wa sukari katika mkojo

CHANGAMOTO

- Upungufu wa watumishi wenye ujuzi mbalimbali wa idara ya Afya kwa asilimia 59.5
 - Uhaba wa dawa na vifaa Tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya.
- Uhaba wa wodi kwa ajili ya kulaza wagonjwa hususani wodi ya wagonjwa wa matatizo ya Akili na kuchakaa kwa rangi za kuta wodi ya watoto,kupasuka kwa kuta za jengo la upasuaji na X-Ray

HALMASHAURI YA MJI KASULU
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Simu/Fax 255-028-2810355



S.L.P. 475.

Mhe: Mwenyekiti

14.11.2017

Mkutano wa Baraza la Madiwani

MJI- KASALU.

**YAH: TAARIFA YA KAMATI YA MIPANGO MIJI, UJENZI NA MAZIINGIRA
KATIKA KIPINDI CHA JULAI-SEPTEMBER (2017/2018).**

Katika kipindi cha mwezi Julai-Septemba 2017, kamati ya Mipango Miji,Ujenzi na Mazingira ilitekeleza shughuli zifuatazo kama zinavyoonekana kwenya hizi Idara zifuatazo.

- Idara ya Ujenzi
- Idara ya Ardhi na Mipango Miji
- Idara ya Usafi na Mazingira

Taarifa kamili imeambatanishwa.

Naomba kuwasilisha.

Mh.Emmanuel Kisunzu

Mwenyekiti

Kamati ya Mipango Miji,Ujenzi na Mazingira

Halmashauri ya Mji- KASULU

Idara ya Mipango Mji

Katika kipindi cha mwezi July -Septemba 2017, Idara ya Ardhi na Mipango Miji imetekeleza kazi mbalimbali kwa kuzingatia mpango kazi wa idara pamoja na maombi mbalimbali kama yalivyowasilishwa na wananchi.

Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

1. Kuchora jumla ya michoro mipya nane (8) ya Mipango Miji katika maeneo ya Malumba (2), Kanazi (1), Heru Juu (1), Kigule (3), Melelani (1).
2. Kutoa masharti ya uendelezaji wa viwanja.
3. Uidhinishaji wa ramani za Majengo kwa wamiliki wa viwanja 30
4. Kutoa elimu ya sheria ya Mipango miji ya namba nane mwaka 2007 Katika Kata ya Kumnyika na Mwilamvya.
5. Kupokea, Kusikiliza na Kutatua migogoro ya Ardhi.
6. Kusimamia zoezi la ukusanyaji wa takwimu za majengo na biashara
7. Kupima viwanja vipya katika eneo mbalimbali ya watu binafsi.
8. Kuandaa ramani 100 za Hati (Deed Plans) za wamiliki wa viwanja vilivyopimwa.
9. Kufanya Uthamini wa mali za watu ili kukopa kwenye taasisi za fedha pamoja na kuhamisha miliki za viwanja.
10. Kukadiria viwango vya kodi za ardhi kwa wamiliki wapya na wale wa zamani.
11. Kuonyesha mipaka ya viwanja na kurudishia alama za upimaji
12. Kuandaa hati Kwa wamiliki wapya wa viwanja
13. kufanya doria na kutoe elimu kwa maeneo yenye misitu.
14. kutembelea na kutoa elimu kwa vikundi vya ufaugaji nyuki.

Kitengo cha Mipango miji na utafiti.

NA	MRADI/SHUGHULI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1.	Kuchora jumla ya michoro mipya nane (8) ya Mipango Miji katika maeneo ya Malumba (2), Kanazi (1),Heru	Michoro 8 yenye viwanja vya matumizi mbalimbali imekamilika na kuwasilishwa kwa katibu tawala mkoa kwa	Michoro itawasilishwa wizara ya ARDHI kwa ajili ya kuidhinishwa.

	Juu (1),Kigule (3), Melelani (1).	ajili ya kukaguliwa.	
2.	Kutoa masharti ya uendelezaji ardhi kwa wamiliki wa viwanja 125 vipya na vile vya zamani.	Jumla ya viwanja 120 vilitolewa masharti ya uendelezaji.	Viwanja vitano havikutolewa masharti kutokana kutokidhi vigezo vya sheria ya Mipango miji ya mwaka 2008
3	Uidhinishaji wa ramani za Majengo kwa wamiliki wa viwanja 27	Jumla ya ramani 27 zilipokelewa na kukaguliwa. Ramani 21 ziliidhinishwa.	Ramani 6 hazikuidhinishwa kutokana na makosa na zimerejeshwa kwa wahusika ili kufanyiwa marekebisho.
4	Kutoa elimu ya sheria ya Mipango miji ya namba nane mwaka 2007 Katika Kata za Kumnyika, Murubona, Murusi, Ruhita na Mwilamvya	Jumla ya kata tatu ambazo ni Kumnyika, Mwilamvya na ruhita elimu ya sheria ya mipango miji namba nane ya mwaka 2007 ilitolewa katika mitaa iliyopo kwenye kata hizo kupitia mikutano.	Elimu inaendelea kutolewa kwenye kata zingine.

2. Kitengo cha Upimaji na Ramani

NA	MRADI/SHUGHULI	HATUA YA UTEKELEZAJI	MAELEZO
1.	Kupima viwanja vipya katika	Jumla ya viwanja 83	Baada ya zoezi la

	eneo mbalimbali ya watu binafsi pamoja na maeneo ya taasisi.	vimepimwa maeneo mbalimbali katika kata za Nyansha, Kimobwa, Mwilamvya, Murusi, Ruhita na Murubona, kati ya viwanja hivyo 72 ni viwanja vya watu binafsi na 11 ni viwanja vya maeneo ya umma.	upimaji, viwanja 54 vimeidhinishwa na wizara ya Ardhi. Viwanja 29 vipo kwenye hatua ya kudhinishwa na Wizara ya Ardhi
1.	Kuonyesha mipaka ya viwanja na kurudishia alama za upimaji zilizoharibika.	Jumla ya viwanja 43 vya wananchi vimebainishwa mipaka yake ikiwa ni pamoja na kurudushiwa alama zake.	Zoezi hili linategemea maombi ya wananchi.
2.	Kuandaa ramani 200 za Hati (Deed Plans) za wamiliki wa viwanja vilivyopimwa.	Jumla ya ramani za hati 155 ziliandaliwa kwa wamiliki mbalimbali wenye viwanja vilivyopimwa upimaji kamilifu ili waweze kuandaliwa hati za kumiliki Ardhi katika kata za Msambara (Kabanga), Heru juu, Murusi, Mwilamvya, Kumsenga, Murubona na Kimobwa.	Uandaaji wa ramani 45 za hati zilizobakia inaendelea na kwa watu wengine ambao wanatuma maombi.
3.	Upimaji wa taasisi za serikali	Jumla ya taasisi 12 za serikali zimepimwa.	Kwakipindi cha Julai-Septemba 2017, jumla ya taasisi 12 za serikali zimepimwa, zikiwemo shule pamoja na zahanati.

3. Kitengo cha Uthamini

NA	MRADI/SHU GHULI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1.	Kuthamini viwanja vilivyohamishwa miliki.	Jumla ya viwanja 17 vimethaminiwa kwaajili ya kuhamishwa miliki	Zoezi hili ni endelevu.
2.	Kukadiria viwango vya kodi za ardhi kwa wamiliki wapya na wale wa zamani.	Jumla ya viwanja 312 vimekadiriwa kodi na wamiliki wamepata bili zao	Zoezi linaendelea.

4. Kitengo cha Ardhi.

NA	MRADI/SHU GHULI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1.	Kuandaa hati kwa wamiliki wapya na wale wazamani.	Jumla ya hati miliki 53 zimeandaliwa.	Hati 42, zimewasilishwa kwa Kamishina na hati 11 bado wamiliki hawajakamilisha taratibu.
2.	Kusimamia uhamishaji miliki za	Jumla ya wananchi 17 wamewasilisha maombi ya kuhamisha miliki zao na	

	ardhi za wananchi.	maombi yote yametekelezwa.	
3	Kusikilizana kutatua migogoro ya ardhi	Taarifa imeambatanishwa	

5. Kitengo cha Maliasili.

NA	MRADI/SHUGHULI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1	Kutoa elimu ya ufugaji wa nyuki kibiashara kwa wafugaji wa nyuki.	<p>Mafunzo yalifanyika kwa siku tano na yaliendeshwa na TANTRADE kuhusu ufugaji wa nyuki kibiashara. Zaidi ya wafugaji 80 walihudhuria mafunzo hayo na kukabidhiwa vyeti vyao. Mafunzo hayoni pamoja na:-</p> <ul style="list-style-type: none"> -Kalenda ya ufugaji na usimamizi wa shamba la nyuki. -Zana za ufugaji nyuki na mizinga bora. -Mchanganuo wa andiko la biashara ufugaji nyuki. -Urasimishaji wa Biashara ya mazao ya nyuki. -Ushiriki wa Maonesho ya Biashara. -Mafunzo ya uchakataji wa Asali na Nta. -Mnyororo wa Thamani. 	

- Menejimenti iliwasilisha maombi ya kutumia kipande cha eneo chenye ukubwa wa ekari hamsini (50) kwaajili ya ujenzi wa chuo cha ualimu. Chuo cha kilimo Mubondo kina eneo lenye ukubwa wa ekari 2011 ambapo eneo linalotarajiwa kujengwa chuo ni eneo ambalo

wananchi walikuwa wanalivamia na kugawana. Hivyo tumeona ni vyema chuo kikajengwa hapo kwa sababu kuu tatu.

1. Eneo hili halihitaji fidia yeyote
2. Eneo hili lina ukubwa wa kutosha hata kama chuo kitapanuka na kuongezwa hadhi kwa miaka baadae.
3. Kuwepo kwa chuo pale kutaondoa kabisa uwepo wa wavamizi. Baada ya mapendekezo hayo kuwasilishwa mbele ya wajumbe wa kikao, wajumbe waliridhia ombi hilo ili michakato ya kuandaa mchoro wa mipango Miji na Upimaji uanze.

IDARA YA UJENZI

Katika kipindi cha utekelezaji wa kazi ya wiki, Idara ya Ujenzi imeendelea kutekeleza majukumu yake katika usimamizi wa Majengo na usimamizi wa matengenezo ya magari na mitambo kama ifuatavyo:-

- Idara ya ujenzi imeendelea kusimamia kwa kutekeleza shughuli za Majengo kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2017, kwa miradi ifuatayo:-
 - a) **KIGOMA GRAND HIGH SCHOOL:-** Kuendelea kufanya ukaguzi wa ujenzi katika majengo **Kigoma Grand High School**, kazi zilizotekelezwa kwa kipindi hicho ni kwa majengo ya Mabweni mawili kwa kumwaga zege la jamvi na nyumba za watumishi na bwalo kwa kumaliza dari na kuanza kusikimu jengo, pia na kuendelea na ukamilishaji wa miundo mbinu mingine, Nyumba ya mkuu wa shule, Madarasa manne, Maabara tatu na Mabweni mawili.
 - b) Shule ya **msingi Mwilamvya**, Ujenzi wa madarasa matatu na Ofisi pia na chuo matundu sita, kazi zilizotekelezwa kuanzia Julai hadi Septemba 2017 madarasa matatu na ofisi ujenzi kuanzia msingi hadi upigaji wa bati na upigaji wa mbao za dari ulikamilika, ikiwa pamoja na upigaji lipu kwa ndani na nje na chuo kilijengwa na kupauliwa vile vile.
 - c) Shule ya **msingi Mwibuye**, Ujenzi wa madarasa matatu na Ofisi pia na chuo matundu sita, kazi zilizotekelezwa kuanzia Julai hadi Septemba 2017, madarasa matatu na ofisi ujenzi kuanzia msingi hadi usawa wa mtambaa panya (ring beam).

na choo kilijengwa hadi usawa wa mtambaa panya na shimo kujengwa hadi usawa wa ardhi.

- d) Shule ya **Sekondari Mubondo**, Ujenzi wa maabara moja hadi kufikia mwishoni mwa rbo ya kwanza Septemba 2017, jengo la Maabara lilikuwa limepauliwa na ukamilishaji wa madarasa matano, yalikuwa yamewekwa zege la jamvi, na madarasa matatu yalikuwa yamepauliwa na yote kupigwa lipu kwa ndani.
- e) Shule ya **Sekondari Muka**, Ujenzi wa madarasa matatu hadi septemba 2017, yalikuwa yamejengwa na kufikia hatua ya kupauliwa yakiwa yanaendelea na kutungiliwa, mabweni mawili yalikuwa yamejengwa kuanzia msingi na kumwagwa zege la jamvi na kuanza ujenzi wa kuta na kufikia usawa wa ring beam. Choo cha wanafunzi matundu sita kilikuwa kimejengwa na kufikia usawa wa mtambaa panya (Ring beam).
- f) Shule ya **Sekondari Bogwe**, Ujenzi wa jengo la Bwalo la chakula hadi kufikia mwezi Septemba 2017, kazi ya ujenzi , zege la jamvi lilikuwa limekamiliwa na kuanza ujenzi wa ukuta.
- g) **Makao makuu ya Halmashauri ya Mji**, Ujenzi kwa eneo hili uchimbaji wa misingi ulikuwa umeanza kwa ajili ya ujenzi wa nguzo.
- h) **Soko la Sofya**, Ujenzi wa soko la Sofya kwa ajili ya ujenzi wa shedi tano, hadi kufiia mwezi Septemba 2017, kazi ya nguzo ilikuwa imeanza na kazi ya uundaji na kuchomelea vyuma vya kenchi inaendelea.

IDARA YA USAFI NA MAZINGIRA

- Idara ya Usafi na Mazingira ina vitengo viwili; Kitengo cha usafi na kitengo cha Mazingira. Kitengo cha Usafi kina majukumu ya kusimamia usafishaji wa mji, ukaguzi wa majengo ya vyakula maeneo ya wazi, mifereji na barabara, utunzaji, uchambuzi na usafirishaji wa taka na kusimamia uendeshaji wa vizimba vya taka. Kitengo cha Mazingira kina majukumu ya kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira (ardhi, vyanzo vya maji, uchafuzi wa mazingira), utunzaji wa mazingirana upandaji miti, majani na maua na kufanya tathmini ya athari za mazingira katika miradi ya maendeleo.
- **Usimamizi wa ukusanyaji na Uzoaji wa taka ngumu kwenye maeneo mbalimbali ya mji wa kasulu**

Kwa kawaida Halmashauri ya mji kasulu inajumla ya wakazi 236,751 hivyo uzalishaji wa taka umefikia tani 18.9 kwa siku na zinazozolewa ni wasta wa tani 5tu kwa siku.

Kwa robo hii ya Julai –septemba 2017 tumefanikiwa kuzoa taka kwa kiasi cha tani 360 ukilinganisha na kiasi cha taka kinacho zalishwa kwa mwezi mmoja ambacho ni tani 529.2

CHANGAMOTO:

- a) Taka ngumu bado zinatupwa ovyo kwenye maeneo yasiyo rasimi.
- b) Ushiriki wa Idara zingine na Jamii , katika ratiba ya usafi wa mazingira siku ya alhamisi na jumaosi ya kila mwisho wa mwezi ni mdogo sana.
- c) Halmashauri kutokuwa na mkakati madhubuti wa pamoja kuhusu usafi na utunzaji wa mazingira.
- d) Ukosefu wa eneo maalumu kwa ajili ya kumwaga taka ngumu
- e) Upungufu wa maeneo maalumu ya kukusanyia taka katika jamii kabla ya kupelekwa kwenye kizimba kikubwa(final disposal point) na kusababisha taka kutupwa ovyo.
- f) Usafiri kwa ajili ya kuzungukia maeneo ni tatizo pia .

UTATUZI WA CHANGAMOTO:

Ili kukabiliana vizuri na swala la usafi na utunzaji wa mazingira changamoto tajwa hapo juu zifanyiwe kazi haraka ili kazi zifanyike kwa usahihi.

3.0 Kitengo cha Mazingira

Katika kipindi hiki cha robo ya kwanza ya Julai - Septemba shughuli zifuatazo zilifanyika:

- Kushiriki katika kampeni ya Usafi wa mazingira wa Mji.
- Ukaguzi wa hifadhi ya vyanzo vya maji.
- Kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira.
- Ukamilishaji wa andiko mradi la kulinda bonde la mto Malagarasi.

3.1 Kushiriki katika kampeni ya Usafi wa mazingira wa Mji

Katika kipindi hiki cha Julai - Septemba Afisa mazingira amekuwa akishirikiana na wadau wote wa usafi wa mazingira kusimamia usafi wa mazingira katika ngazi za kata, taasisi na maeneo ya umma. Aidha Afisa mazingira ni msimamizi wa usafi wa mazingira katika kata ya Mwilamvya, kazi ambayo imekuwa ikifanyika kwa ushirikiano wa karibu na viongozi wa kata.

3.2 Ukaguzi wa hifadhi ya vyanzo vya maji.

Kwa kushirikiana na wataalam kutoka idara za maji na maliasili, kitengo cha mazingira katika kipindi hiki kimeweza kufanya ukaguzi na kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya vyanzo vya maji katika maeneo ya Kumnyika, Marumba, Kumsenga na Heru Juu (mtaa wa Tulieni). Zoezi hili

liliambatana na kutoa maelekezo ya kusitisha shughuli zote za ujenzi, kilimo, uchimbaji wa madini ya mchanga na kokoto na kukata na kuangamiza miti ya mikaratusi ilipandwa katika hifadhi ya vyanzo vya maji.

3.3 Kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira

Katika kipindi hiki cha Julai – Septemba, elimu ya hifadhi ya mazingira imetolewa kupitia mikutano ya hadhara iliyofanyika katika maeneo ya Kumnyika, Mwilamvya, Kumsenga na Marumba. Aidha wakulima katika chanzo cha maji cha mto chai kutoka mtaa wa Tulieni kata ya Heru Juu na vikundi vya wanajamii wanao jitolea (volunteers) kutoka kata za Mhunga na Kumsenga wameelimishwa juu ya athari za uharibifu wa mazingira, mbinu na faida za utunzaji wa mazingira hususan hifadhi ya vyanzo vya maji.

3.1 Ukamilishaji wa andiko mradi la kulinda bonde la mto Malagarasi, mto Ruaha na ziwa Rukwa.

Kitengo cha mazingira katika robo hii ya Julai – Septemba kimeendelea kushirikiana na ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kukamilisha andiko mradi wa kuhifadhi bonde la Mto Malagarasi, mto Ruaha na ziwa Rukwa. Mradi huu unaotarajiwa kuanza Januari, 2018 utatekelezwa katika wilaya nane (8) za Tanzania bara katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya (Bonde la mto Ruaha), Rukwa na Katavi (Bonde la ziwa Rukwa) na Katavi na Kigoma (Bonde la mto Malagarasi). Aidha katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu mradi huu unalenga kutekelezwa katika kata ya Msambara ambapo mto Ruchugi unaoingiza maji yake katika mto Malagarasi umeanzia.

MIKAKATI YA KITENGO CHA MAZINGIRA:

- i. Kitengo cha mazingira kusimamia kikamilifu zoezi la kukata na kuangamiza miti ya mikaratusi katika vyanzo vyote vya maji Halmashauri ya Mji wa Kasulu.
- ii. Kitengo cha mazingira kwa kushirikiana na vitengo na idara husika kuelimisha wananchi wa Mji wa Kasulu juu ya miongozo, taratibu, kanuni na sheria zinazosimamia hifadhi ya mazingira kupitia vikundi, jumua na mikutano ya hadhara.
- iii. Kitengo cha mazingira kuhamasisha na kushirikiana na wadau mbalimbali wa uhifadhi wa mazingira kuandika maandiko mradi ya hifadhi ya mazingira.

HALMASHAURI YA MJI KASULU
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Simu/Fax 255-028-2810355



S.L.P. 475.

Kumb . Na. KTC/T.2/1/16

14.10.2017

Mhe: Mwenyekiti

Mkutano wa Baraza la Madiwani

MJI- KASALU.

YAH: TAARIFA YA KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JULAI-SEPTEMBER 2017/2018).

Katika kipindi cha mwezi Julai-Septemba **2017/2018** , kamati ya **KUDHIBITI UKIMWI** ilitekeleza shughuli mbalimbali kama inavyoonyeshwa kwenye taarifa hii iliyoambatanishwa.

Taarifa kamili imeambatanishwa.

Naomba kuwasilisha.

Mh.Deus Kibabi

Mwenyekiti

Kamati ya Kudhibiti Ukimwi

Halmashauri ya Mji- KASULU

UTANGULIZI:

Shughuli za kuzuia na kudhibiti Ukimwi ziliendelea kutolewa kama kawaida. Katika kipindi hiki shughuli zifuatazo zilitekelezwa.

MJI

1. Ushauri na upimaji wa hiari (**VCT**) – (Voluntary Counseling and Testing)
2. Kutoa huduma za ushauri na upimaji zinazoanzishwa na kuchochewa na watoa huduma wa afya (Providerr Initiated Testing and Counseling) (**PITC**)
3. Huduma ya Tiba, uangalizi na ufuatiliaji kwa wagonjwa wenye maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (Care and Treatment)
4. Huduma ya kuzuia maambukizi ya **VVU** kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, (Prevention of HIV from Mother to Child Transmission) (**PMTCT**)
5. Huduma za ugunduzi wa awali wa mtoto waliozaliwa na mama wenye maambukizi **VVU/UKIMWI** chini ya miezi 18 (Early Infant Diagnosis)(**EID**)
6. Utoaji wa huduma kwa wagonjwa majumbani hasa wale wenye magonjwa ya kusendeka (Home Based Care(**HBC**))
7. Kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma za Afya kuhusu huduma stahili kwa watu walio na maambukizi ya **VVU/UKIMWI** (Capacity Building)
8. Kutoa huduma shirikishi za kifua kikuu na **UKIMWI** (**TB/HIV**)
9. Kutoa huduma kwa wagonjwa wa magonjwa ya ngono na via vya uzazi (**STI/RTI**)
10. Kuendelea kuelimisha jamii kuhusu kujikinga na maambukizi ya **VVU** na huduma zinazotolewa kwa mtu anayegunduliwa kuwa na maambikizi ya **VVU** na mahali huduma hizo zinapopatikana.

HALI HALISI YA UTEKELEZAJI:

Jumla ya watu **9200** walipima Afya zao **ME 3000 KE 6200** kwa njia mbalimbali kupitia vitengo vya **VCT, PMTCT, PITC**. Kati ya waliopima waliogunduliwa kuwa na maambukizi walikuwa **60 (ME 15, KE 45)** (sawa na asilimia **0.6%**)

HUDUMA ZA USHAURI NASAHA NA UPIMAJI WA VVU: (VCT)

Huduma hii inaendelea kutolewa katika vituo 4 ambavyo ni: - Hospitali ya Halmashauri ya Mji, Kabanga, kituo cha Afya Kiganamo,Ruhita.

MCHANGANUO WAKE NI KAMA ILIVYOAINISHWA KWENYE JEDWALI LIFUATALO:-

TAKWIMU ZA HUDUMA ZA UPIMAJI VVU

UMRI 15- zaidi	WALIOPIMA			WENYE MAAMBUKIZI			KIWANGO 2.2%
	ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA	
JUMLA	244	245	489	1	10	11	

HUDUMA ZA USHAURI NASAHA NA UPIMAJI WA VVU ZINAZOANZISHWA NA WATOA HUDUMA WA AFYA – (PITC)

Huduma hii iliendelea kutolewa katika vituo 5 ambavyo ni: - Hospitali ya Halmashauri ya Mji, Hospitali ya Kabanga, vituo vya Afya vya Kiganamo, Kigondo, Herujuu.

TAKWIMU ZA HUDUMA ZA UPIMAJI

UMRI Miezi 18 na zaidi	WALIOPIMA			WENYE MAAMBUKIZI			KIWANGO 0.7%
	ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA	
JUMLA	2228	3748	5976	15	26	41	

HUDUMA ZA KUZUIA MAAMBUKIZI KUTOKA KWA MAMA KWENDA KWA MTOTO (PMTCT)

Huduma hizi zinaendelea kutolewa katika vituo 14 hapa Halmashauri ya Mji. Vituo hivyo ni: - Kasulu Hospitali ya mji, Kabanga Hospitali, Kiganamo, Msambara, Mwanga, Mwibuye, Herujuu, Muhunga, Marumba, Nyumbigwa, Kigondo, Kidyama, Ruhita, Kanazi, Murufiti

HALI YA UTEKELEZAJI

UMRI 15-49	WALIOUDHURIA			WALIOPIMA			WENYE MAAMBUKIZI			KIWANGO 0.45%
	ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA	
	1870	2282	4152	1870	2220	4090	4	10	14	
JUMLA										

HUDUMA YA TIBA, UANGALIZI, USIMAMIZI NA UFUATILIAJI (CTC)

Huduma hii iliendelea kutolewa katika vituo 3 ambavyo ni: - Hospitali ya Halmashauri ya Mji, Kabanga na Kituo cha Afya Kiganamo.

HALI HALISI YA TIBA KWA WENYE VVU/UKIMWI

KITUO	UMRI	WALIOANDIKISHWA			WANAOTUMIA ARV			KIWANGO
		ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA	

Kabanga	>14 <14	91 8	236 17	327 25	54 7	167 8	221 15	%
Kiganamo	>14 <14	67 7	375 11	42 18	47 7	337 9	384 16	
Kasulu Hospitali ya Mji	>14 <14	712 109	1513 121	2225 230	553 89	1142 90	1695 179	
JUMLA		994	2273	3267	753	1753	2510	

HUDUMA YA TIBA NA USHAURI NASAHA MAJUMBANI

Huduma hizi zinaendele kutolewa katika vituo 14 hapa wilayani ambavyo Ni:-

Kasulu Hospitali ya mji, Kabanga Hospitali, Kiganamo, Msambara,

Mwanga, Mwibuye, Herujuu, Muhunga, Marumba, Nyumbigwa, Kigondo, Kidyama, Ruhita, Kanazi

JEDWALI LINALOONYESHA WAGONJWA WALIOPATA HUDUMA HIZO:-

WALIOPATA HUDUMA			VIFO		
ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA
276	1000	1276	5	6	11

HUDUMA ZA TIBA KWA MAGONJWA YANAYOAMBUKIZWA KWA NJIA YA NGONO.

Huduma hii iliendelea kutolewa katika vituo 14 vilivyopo wilayani ambavyo ni: - Hospitali ya Halmashauri ya Mji, Hospitali ya Kabanga, Vituo vya Afya vya: -

Kiganamo, Msambara, Mwanga, Mwibuye, Herujuu, Muhunga, Marumba, Nyumbigwa, Kigondo, Kidyama, Ruhita, Kanazi.

UMRI 15-na zaidi	IDADI YA WALIOAMBUKIZWA		JUMLA	WALIOSHAURIWA NA KUCHUKUA KONDOMU	
	ME	KE	JUMLA	ME	KE
GDS	48	680	728	60	109
GUD	4	7	11		
PID	0	1519	1519		
OTHER STI	21	51	72		
JUMLA	73	2257	2330		169

HUDUMA SHIRIKISHI YA KIFUA KIKUU NA UKIMWI

Huduma hii inaendelea kutolewa katika vituo 4 ambavyo Ni: - **Hospitali ya wilaya Kasulu, Kabanga, Kiganamo Kituo cha Afya na Zahanati ya Msambara.**

TAKWIMU ZA WALIOPATA HUDUMA HIZO:-

- Wagonjwa wapya wa kifua kikuu **37 (ME 27 KE 10)**
- Wagonjwa wenye Kifua Kikuu na **UKIMWI 4 (ME 2, KE 2,)**
- Wagonjwa wa kifua kikuu waliopima maambukizi ya virusi vya **UKIMWI 27 (ME 21, KE 6)** waliobainika kuwa na **VVU 4 Me 2 Ke 2.**

MAFANIKIO:

- Watu wengi wanaendelea kuhamasika kupima Afya zao.
- Wanaume wanaendelea kuongezeka katika huduma za kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.
- Watoa huduma wa Afya katika vituo vya kutolea huduma wanaendelea kujengewa uwezo kwa kufundishwa mambo mbalimbali ili waweze kutoa huduma vituoni ikiwa ni pamoja na Elimu katika maeneo ya kazi.
- Wataalamu kutoka shirika la thps wanatutembelea mara kwa mara kuwaelekeza watumishi wetu mambo mbalimbali ili kuboresha huduma za ukimwi katika viyuo vyetu
- Tumeshafanya utambuzi na kuteua vituo vinavyofaa kwa ajili ya kutolea huduma za ukimwi,ikiwemo kutoa dawa za kufubaza makali.hivyo tutaongeza vituo vya huduma.
- Maabara yetu imekuwa kituo kikuu cha kukusanyia sampuli za viral load(wingi wa virusi)kwa kibondo,kasulu dc na kasulu tc ili kupelekwa lugalo dar kupimwa na imeendelea kufanya vizuri.
- Tumepokea vifaa kama makabati mapya kutoka **THPS** kwa ajili ya kutunzia mafaili na takwimu mbalimbali za wagonjwa.
- Tumepatiwa mafunzo mbalimbali ya kujengea watumishi wa kitengo cha CTC uwezo wa kitaalamu juu ya ukimwi na magonjwa nyemelezi
- THPS wameendelea kukarabati jingo la **CTC** na kwa sasa wanajenga sehemu maalumu kwajili ya kuchezea watoto wanapokuja kiliniki.
- Mikutano ya pamoja kwa waratibu wa ukimwi wa halmashauri mbalimbali ili kubadilishana uzoefu wa utoaji huduma
- Tumeanzisha kliniki tembezi(mobile clinic)kwa vituo vyetu vyote vya serikali,ambapo tunaenda kutoa dawa za kuifubaza virusi kila mwezi ili kupunguzia wananchi umbali wa kufuata huduma hizo hospitali ya Kasulu na Kiganamo.
- Tumekua na hema tuliloliweka karibu na geti la hospitali lenye vifaa vyote kwa ajili ya kupima maambukizi ya ukimwi kwa hiari wagojwa na watu wote wanaoingia na kutoka hospitalini(**PITC**)

CHANGAMOTO:

- Tulikuwa na upungufu wa dawa za Magonjwa nyemelezi
- Upungufu wa fedha ya kuendesha Kliniki ya vijana kutokana na upungufu huo vijana wanakosa kushirikiana na vijana wenzao Katika vituo vingine.

- Upungufu mkubwa wa watumishi katika kitengo cha CTC
- Upungufu wa vitendea kazi ambao sasa thps wanajitahidi kutufadhili
- bado hatujapata mbadala wa TACC kutokana na upungufu mkubwa wa watumishi katika halmashauri.

MIKAKATI:

- Kuhakikisha dawa za Magonjwa nyemelezi zinapatikana mda wote kupitia MSD na wadau wa THPS
- Kuwasiliana na wadau mbalimbali wa Ukimwi ili kupata fedha za kuendeshea Kliniki za vijana ili waweze kushiriki warsha mbalimbali.